# DHAMIRA YA UOZO NA ATHARI ZAKE KWA JAMII, KATIKA RIWAYA YA UPOTEVU

**NA**

**JONES N. MANOTI**

**C50/66093/2010**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**NOVEMBA 2012**

University of NAIROBI Library

0389224 7

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili katika chuo kingine chochote.

-------------------------------------- 02.11.2012

**Jones Manoti** **Tarehe**

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

-------------------------------------- 8-11-2012

**Prof. K. W. Wamitila** **Tarehe**

-------------------------------------- 02/11/2012

**Dkt. Mwangangi wa Musyoka** **Tarehe**

# TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa wazazi wangu walioniwekea msingi wa masomo. Mama Truphena Mong'ina kwa bidii zake za kunilea, kunielimisha, kuniendeleza, kunifunza haja ya uvumilivu maishani, kuniunga mkono na kunishauri kwa lolote nililoazimu kulifanya. Baba Wilson Manoti kwa kuwa kielelezo bora, kunifunza umuhimu wa elimu maishani na kwa maazimio mema aliyokuwa nayo ambayo yalikatizwa na mkono wa kifo.

# SHUKRANI

Ninakiri kwamba kazi hii haingeweza kukamilika bila ya usaidizi, uongozi na mchango wa watu wengi. Ni vigumu kuwataja wote; hata hivyo, nitawataja wachache.

Kwanza, ningependa kutoa shukrani maalum kwa Prof. K. W. Wamitila kwa mawaidha na ushauri wake wa busara, mwongozo na masahihisho aliyonipatia wakati ningali katika vuguvugu la kutofahamu ni njia ipi nitakayoifuata katika bahari hii ya usomi na utafiti. Kama msimamizi wangu, hakuchoka kusoma kazi yangu kila nilipompelekea na kunishauri ipasavyo. Ninampongeza kwa namna alivyopitia sehemu mbalimbali za kazi yangu kwa haraka na kwa umakini na kuniwezesha kukamilisha utafiti wangu kwa wakati. Mawaidha yake mema hasa kuhusu jinsi ya kuandika na kuipanga kazi ya kitaalamu yalinitia ari na mshawasha wa kuwaza zaidi katika kuboresha kazi hii.

Shukrani zangu za dhati nazitoa pia kwa Dkt. Mwangangi wa Musyoka ambaye hakuchoka kusoma maoni yangu mara kwa mara. Uhakiki wake wa maoni yangu, motisha, mapendekezo na mwongozo; mambo yote haya yalinifaa pakubwa katika kuikamilisha tasnifu hii. kwa maongezi yake kama msimamizi wangu, namshukuru.

Shukrani zangu pia ziwaendee wahadhiri walionifunza katika Idara ya Isimu na Lugha ya Chuo Kikuu cha Nairobi. Ahsante kwa kunisaidia, kuniongoza na kunielekeza katika safari hii ya usomi ambayo haikuwa rahisi. Hawa ni: Prof. John Habwe, Prof. Kineene wa Mutiso, Dkt. Iribe Mwangi, Dkt. Omboga Zaja, Dkt. Mwenda Mbatiah, Dkt. Evans Mbuthia, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Amri Swaleh na Bw. Basilio Mungania.

Kamwe sitawasahau wenzangu ambao tuliabiri jahazi moja la kutafuta shahada ya uzamili na kuhakikisha tumefika mwisho wa safari licha ya mawimbi makali baharini. Tulipitia mengi ambayo yalikuwa ya kututia moyo na wakati mwingine tukivunjika moyo lakini tulihimizana na kusaidiana kwa vyovyote vile ili kuhakikisha kuwa hakuna mmoja wetu angelemewa na safari hii. Tuliokuwa nao katika darasa la Kiswahili ni pamoja na: Modgen Chisia, David Bore, Pauline Rono, Nixon Migiro, Geoffrey Gatakaa, Dorine Mboti, Monica Cherop, Samson Otwere, Janet Mwende, Charles Ndege, Joyce Onyoni, Grace Mjomba, Kenguru

Maina, Jacklyne Kavivi, Jenipher Oyoyo, Elijah Obure, Omar Said, Rael Onchangu, Benard Achieng, Leah Gatimu, Sabastian Mutswenje, Ruth Naliaka, Timothy Kiunga na Florence Njoroge. Hongera kwenu nyote kwa juhudi zenu. Nawaombea dua njema mfanikiwe katika kila mlitendalo.

Sitamsahau mke wangu mpenzi, Mary Kemuma. Namuwia shukrani za kipekee. Usaidizi wake ndio ulioniwezesha kuianza, kuiendeleza na kuitimiza safari hii. Nasema ahsanteni kwa uvumilivu wako mwingi wakati nikishughulika katika safari nzito ambayo uliielewa na kunitakia ufanisi. Shukrani pia kwa kuipiga chapa tasnifu hii.

Nawasheheshea shukrani za dhati ya moyo wangu ndugu yangu Stephen Manoti na mke wake Druscillah Moraa walionihimiza wakati wote nikizama na kuibuka katika bahari hii ya usomi. Nawatakia kila la kheri maishani mwao.

Nawashukuru marafiki na jamaa ambao walipojua ninaendelea na masomo, walinitia moyo na kunihimiza kuendelea. Nitaanza na Mwalimu Mkuu Bw. David M. Onyango aliyenionyesha moyo wa wema na hekima, na kila mara alinielekeza na kunipa ushauri tosha juu ya maswala muhimu yaliyohusiana na masomo yangu. Wengine ni pamoja na: Meshack Nyagwa, Joseph Arogo, Benard Simwamu, Zacharia Momanyi na Job Isoe.

Hawa wote niliowataja na wengine ambao sikuwataja nawashukuru kwa kunifaa katika kufanikisha kazi hii. Na mwisho, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa mapenzi yake yaliyoniwezesha kufikia kiwango hiki.

# IKISIRI

Utafiti huu ulishughulikia dhamira ya uozo na athari zake kwa jamii, katika riwaya ya *Upotevu* ya Mwenda Mbatiah.

Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa kuchanganua dhamira ya uozo katika riwaya ya *Upotevu,* kuchunguza uhusika unavyotumiwa kuendeleza uovu na kuonyesha madhara ya uovu katika jamii.

Kazi hii ina sura tano. Katika sura ya kwanza, tumetoa pendekezo la utafiti linalojumulisha tatizo la utafiti na kuorodhesha madhumuni na nadharia tete za utafiti huu. Katika sura hii pia tulishughulikia sababu za kuchagua mada, upeo wa utafiti, msingi wa nadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada na njia za utafiti. Tulitumia mbinu ya maktabani katika kukusanya data tuliyohitaji na kuichanganua.

Katika kazi hii, tulitumia nadharia ya Maadili kwa sababu riwaya hii ya *Upotevu* ina maudhui mengi yanayodhihirisha ukiukaji wa maadili katika jamii.

Katika sura ya pili, tulishughulikia dhamira ya uozo katika riwaya ya *Upotevu.* Waaidha, sura ya tatu imechunguza namna uhusika ulivyotumiwa kuendeleza uovu. Tumezungumzia wahusika wa kitaashira wenye matendo mema na maovu.

Katika sura ya nne, tumebainisha madhara ya uozo katika jamii kwa kurejelea kikamilifu riwaya ya *Upotevu.*

Sura ya tano ni hitimisho. Katika sura hii tumetoa maoni kuhusu tasnifu hii pamoja na mapendekezo ya kufanya kwa utafiti zaidi.

# YALIYOMO


**U.k**

Mada ---------------------------------------------------------------------------------------------- i

Ungamo ------------------------------------------------------------------------------------------ ii

Tabaruku ------------------------------------------------------------------------------------------ iii

Shukrani ------------------------------------------------------------------------------------------ iv

Yaliyomo ------------------------------------------------------------------------------------------ vi

Orodha ya vifupisho -------------------------------------------------------------------------- ix

## SURA YA KWANZA

## PENDEKEZO LA UTAFITI

1.0.0 Utangulizi ------------------------------------------------------------------------------ 1

1.0.1 Dhamira -------------------------------------------------------------------------------- 2

1.0.2 Uovu ------------------------------------------------------------------------------------ 3

1.0.3 Mwandishi wa *Upotevu* ------------------------------------------------------------- 7

1.1.0 Tatizo la Utafiti ----------------------------------------------------------------------- 8

1.2.0 Madhumuni ya Utafiti ---------------------------------------------------------------- 8

1.3.0 Sababu za kuchagua mada ------------------------------------------------------------ 9

1.4.0 Upeo na Mipaka ya Utafiti ----------------------------------------------------------- 9

1.5.0 Nadharia Tete -------------------------------------------------------------------------- 10

1.6.0 Msingi wa Kinadharia ---------------------------------------------------------------- 10

1.7.0 Yaliyoandikwa Kuhusu Somo Hili ------------------------------------------------- 15

1.8.0 Njia za Utafiti ------------------------------------------------------------------------- 19

## SURA YA PILI

## DHAMIRA YA UOZO KATIKA RIWAYA YA *UPOTEVU*


2.0.0 Utangulizi ---------- 20

2.1.0 Uozo Katika Jamii ---------- 20

2.1.1 Ufisadi ---------- 21

2.1.2 Dhuluma ---------- 23

2.1.3 Anasa ---------- 26

2.1.4 Ukoloni na Ukoloni Mamboleo ---------- 31

2.1.5 Wivu ---------- 33

2.1.6 Ulevi ---------- 35

2.1.7 Tamaa ---------- 37

2.1.8 Elimu na Utamaduni ---------- 38

2.2.0 Hitimisho ---------- 41


## SURA YA TATU

## UHUSIKA ULIVYOTUMIWA KUENDELEZA UOVU


3.0.0 Utangulizi ---------- 42

3.1.0 Wahusika Waovu Katika Riwaya ya *Upotevu* ---------- 45

3.2.0 Wahusika Wema Katika Riwaya ya *Upotevu* ---------- 58

3.3.0 Hitimisho ---------- 65

## SURA YA NNE

## ATHARI ZA UOVU KATIKA JAMII

4.0.0 Utangulizi ---------- 67

4.1.0 Utabaka na Umaskini - ---------- 68

4.2.0 Vifo ---------- 73

4.3.0 Hofu ya Kimaisha ---------- 78

4.4.0 Athari za Ukoloni ---------- 80

4.5.0 Kutowajibika ---------- 82

4.6.0 Magonjwa ---------- 89

4.7.0 Vita ---------- 90

4.8.0 Kukata Tamaa ---------- 91

4.9.0 Hitimisho ---------- 93

## SURA YA TANO

## HITIMISHO

5.0.0 Utangulizi ---------- 95

5.1.0 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti ---------- 95

5.2.0 Ufaafu wa Kinadharia ---------- 98

5.3.0 Tafiti za Baadaye ---------- 99

MAREJELEO ---------- 101

# ORODHA YA VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| Dkt. | - | Daktari |
| K.h.j. | - | Kama hapo juu |
| K.v. | - | Kama vile |
| N.k. | - | Na kadhalika |
| Prof. | - | Profesa |
| TUKI | - | Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili |
| U.k | - | Ukurasa |

# SURA YA KWANZA

## 1.0.0 UTANGULIZI

Katika utafiti huu, tunashughulikia dhamira ya uozo na athari zake kwa jamii katika riwaya ya *Upotevu.*

Kazi ya kifasihi hutungwa katika muktadha wa jamii maalum ili kuonyesha welewa na utambuzi wa mitagusano na matukio ya jamii hiyo. Kwa mujibu wa Kimani na Chimerah, (1999:28), kabla msanii hajazama katika uhalisi wa kilimwengu, chanzo chake huwa ni jamii fulani finyu. Hali zilizoikumba jamii hiyo hupewa muktadha mpana ili zisigubike jamii pana. Aidha, sanaa yote nzuri huibuka katika hali fulani mahsusi, lakini papo ina matokeo ya kiulimwengu. Yaani, tokeo katika jamii huweza kufahamika katika jamii nyingine ambayo huenda haikuchangia katika uibushaji wa kazi hiyo ya fasihi. Vile vile, fasihi hulenga katika kumpanua msomaji mawazo. Hujaribu pia kumulika uhalisia kama unavyoeleweka na msanii. Riwaya kama utanzu mojawapo katika tanzu za kifasihi, inatekeleza majukumu haya ya kifasihi.

Maisha katika jamii inayosawiriwa na mwandishi wa riwaya ya *Upotevu* ni mfano wa maisha yanayoweza kupatikana katika jamii zote za kilimwengu na wananchi wanatahadharishwa kugutuka na kuyatathmini maisha yao upya katika harakati zao za kujikomboa kutokana na mitego ya upotevu.

### 1.0.1 **Dhamira**

Wamitila (2003:33), anasema kuwa dhana ya dhamira hutumiwa kueleza wazo kuu katika hadithi au riwaya, tamthilia, hadithi fupi, shairi na kadhalika. Wazo hilo kuu huhusiana na lengo la mwandishi wa kazi hiyo au huweza kutumiwa kueleza lengo kuu la utunzi. Ni suala linalokuzwa na kuendelezwa na msuko pamoja na mahusiano ya wahusika mbalimbali katika kazi ya kifasihi.

Kimani na Chimerah (1999:23), wanaeleza maana ya dhamira kama shabaha ya kazi ya fasihi. Dhamira hiyo hutuelekeza katika shabaha inayobainika, tangu mwanzo hadi mwisho wa kazi ya fasihi.

Kila kazi ya kifasihi inapaswa kuwa na jambo ilisemalo na lililokuzwa na kujitokeza kwa njia inayotambulikana. Tukiegemea kwenye kauli hii pamoja na fasili zilizotolewa hapo juu, tunaweza kusema kuwa dhamira ni wazo kuu linaloitawala kazi ya kifasihi kuanzia mwanzo mpaka mwisho. Wazo hili hukuzwa kwa njia zilizo wazi kama vile kuwa na wahusika wanaoendeleza wazo hilo tangu mwanzo hadi mwisho wa kazi lengwa.

Dhamira ya riwaya ya *Upotevu* ni ubainishaji wa matendo maovu katika jamii inayosawiriwa na mwandishi. Kupitia kwa mhusika Kemathi na wenzake, mwandishi anatueleza kuhusu wasomi wanaongojewa na jamii kuipa mwelekeo kutokana na elimu yao. Wahusika hao wanapambana na matatizo ya kibinafsi na ya kijamii huku hatima yake ikiwa ni kuzama vilivyo katika uozo wa kila namna na madhara yake hayawezi kuepukika.

Mbatiah, kwa kutumia wahusika kama Chabare, Flora, Mbaabu, Muthomi na wengine, anatuonyesha matendo ya upotevu kwa kina. Maovu hayo yanakithiri na kuonekana

kukomaa na kuzaa maovu mengine zaidi. Kwa hivyo, itaonekana kwamba dhamira ni sehemu ya maudhui, na inatuelekeza katika shabaha inayobainika tangu mwanzo hadi mwisho.

### 1.0.2 **Uovu**

Uovu katika upana wake unaweza kuelezwa kama ukiukaji wa yale yanayochukuliwa kuwa matendo mema. Ukosefu wa wema katika maisha. Uovu, kulingana na mtazamo wa maisha bora ya binadamu, ni yale ambayo hayafai kuwepo. Hata hivyo, hakuna sehemu ya maisha ya mwanadamu ambayo uovu haujitokezi.

Uovu unaweza pia kufafanuliwa kama viwango dhahiri vya mienendo miongoni mwa watu, ambamo matendo hayo huchukuliwa kuwa mabaya na yenye kukosa uadilifu. Ni hali ya kutenda mabaya au ubatili wa matendo ya binadamu. Katika fasili hii, Uovu unahusishwa na binadamu kwa sababu ya uwezo wake wa kuyajali au kutoyajali maslahi ya mwenzake. Kwa kuhakikisha kuwa watu wanatoa huduma zinazofaa, jamii huwa imetoa kanuni zinazoelekeza mienendo katika jamii. Kanuni hizo zina uwezo wa kuyakubali na kupiga marufuku matendo fulani. Yale matendo yanayopigwa marufuku ni yale yanayofikiriwa kukatiza furaha na kusababisha huzuni kwa mtu binafsi au kwa wengine.

Kulingana na hali ya uovu, ni muhali kutambua kwamba uovu unaweza kugawika katika makundi kama vile; uovu wa kimatendo, uovu wa kiadili, uovu wa kimetafizikia, uovu wa mwonoulimwengu na uovu wa kijamii.

Uovu wa kimatendo unajumuisha yale yote ambayo huweza kumdhuru mwanadamu kimwili, kisaikolojia au kukwaza uwezo wake wa kujiendeleza kama mtu binafsi au yeye na

mahusiano yake na maisha ya kila siku. Mifano ya uovu wa kimatendo ni kama dhuluma, ajali, mauaji, umaskini, magonjwa, kusumbuka kiakili kama vile kuudhika, kufedheheka, kukata tamaa na mapuuza.

Uovu wa kiadili ni aina ya uovu unaohusishwa na nyanja za kidini. Ni uovu unaoegemezwa katika matendo yanayokwenda kinyume na mapenzi ya Mungu. Kuamini kuwa nia hutolewa na dini. Ukiukaji wa kanuni au sheria ziongozazo dini. Vitendo vinavyotokana na kuasi kunaofungamana na maswala ya dini. Msimamo hapa ni kwamba utashi wa kuchagua ndio unaopaswa kudhibiti tabia ya matukio na sio matukio kudhibiti tabia ya binadamu. Biblia inataja aina hii ya uovu kuwa ni ile hali ya kutanga mbali na Mungu au kukataa mapenzi ya Mungu. Umejengeka katika misingi ya imani kuwa Mungu aliweka sheria zinazoongoza ulimwengu. Mifano hapa ni uzinzi, wivu, na wizi.

Uovu wa kimetafizikia huletwa na majanga ya ghafla. Viumbe, wanyama na mimea husukumwa na hali ya hewa na mengine na kusababisha maovu. Ni uovu ambao hauhusishwi na matendo ya binadamu kwa sababu hausababishwi naye. Uovu wa kimetafizikia huwa tu na waathiriwa na huletwa na matukio yasiyodhibitiwa na mwanadamu. Mifano hapa ni mitetemeko ya ardhi, mikasa ya moto, magonjwa kama saratani, na mafuriko.

Uovu wa Mwonoulimwengu. Dhana ya 'uwepo wa uovu katika ulimwengu' imekuwa swala la mjadala kwa wasomi kwa karne nyingi. Nadharia nyingi zimeibushwa kujaribu kueleza ukweli wa dhana ya uovu ikihusishwa na uwepo au kutowepo kwa Mungu. Waaidha, uovu kimwonoulimwengu ni dhana yenye utata kubaini kwa kuzingatia ukweli kwamba kila jamii ina kanununi zake ambazo kwazo kitendo chaweza kusemwa kuwa kiovu au kizuri. Pia, kuna

uwezekano wa kitendo fulani kiovu katika jamii fulani kusemwa kuwa kitendo kizuri katika jamii nyingine.

Hata hivyo, kuna juhudi za kutafuta maafikiano baina ya binadamu wote kuhusu kile ambacho kinaweza kuitwa uadilifu au uovu. Swali kuu tunalojiuliza hapa ni je, kuna fasili bia ya dhana ya uovu?, au uovu unafafanuliwa tu kwa misingi ya tamaduni na desturi za jamii fulani. Uovu basi katika muktadha huu unaweza kufasiliwa kama ukiukaji wa kanuni zinazoelekeza na kudhibiti mienendo katika jamii pana ya kilimwengu. Ni ukosefu wa uadilifu na yale yote ambayo yanaweza kuvuruga amani, kudhuru, fadhaisha na hata kuumiza. Kuna vitendo ambavyo vinaweza kuchukuliwa kuwa viovu kilimwengu, navyo ni kama ubakaji, ugaidi (terrorism), mauaji na uangamizaji (genocide).

Uovu wa kijamii (social evils), ni aina ya matendo yanayopingana na wema. Matendo ambayo hayakubaliwi na jamii na ambayo yanaweza kusababisha uchungu na mateso. Mifano: Uhalifu, elimu potofu, ukatili, dhuluma, vitisho, ubaguzi, tamaa, chuki, wivu, na ukandamizaji.

Kutokana na fasili za hapo juu, tunaweza kugawa uovu katika makundi mawili kuu kwa misingi ya chanzo chake: Uovu wa kiadili, na uovu asilia. Phillps et al (2008) anatambua uovu wa kiadili kama vitendo viovu vinaosababishwa na maamuzi ya hiari ya binadamu. Uovu asilia ni uovu ambao haunasibishwi na vitendo vya binadamu. Yaani ni uovu unaoletwa na majanga ya ghafla yasiyodhibitiwa na binadamu. Mifano ya uovu wa aina hii ni mitetemeko ya ardhi na kimbunga au tufani.

Hata hivyo, makundi haya yote ya uovu yana ugilili au mwingiliano wa kiasi fulani hivi kwamba ni vigumu kutenga kundi fulani la uovu kabisa na makundi mengine. Tunaweza kuhitimisha sehemu hii kwa kukubaliana kwamba uovu wa aina yoyote una athari hasi na si chanya. Uovu haumletei mtu chochote kizuri ila husababisha uchungu, mateso, fadhaa na kukosa furaha. Kwa hivyo, unafaa kuepukwa.

Katika riwaya ya *Upotevu,* tunadhamiria kuichunguza dhana ya uovu katika upana wake ili kujumlisha: ufisadi, dhuluma, anasa, ukoloni na ukoloni mamboleo, wivu, ulevi, tamaa, elimu na utamaduni.

Mwandishi wa riwaya ya *Upotevu* anatusawiria jamii inayodhihirisha uhaba wa uadilifu na imo katika upotevu. Mtunzi anasimulia kwamba katika jamii hiyo, visima vya maadili vimeshakauka na nchi ikawa jangwa lililotapakaa ubinafsi na uroho. Anasema: "Maadili hayamei katika jangwa bali huhitaji rutuba ya uongozi bora na kupaliliwa kwa malezi mema." (uk. 144).

Vitu hivyo vimesahaulika kabisa kwa sababu ya usaliti wa kisiasa, utabaka, uporaji wa mali ya umma na ukosefu wa vielelezo vya uadilifu. Katika jamii hii, tunaelezwa kwamba wezi watazaa wezi na waongo watazaa waongo kwa sababu mtoto wa nyoka ni nyoka.
Hatimaye, maovu hayo hukithiri na kupewa hadhi, anavyosema mwandishi kwamba; "ukware sasa umepewa hadhi ya digrii ya chuo kikuu. Ukware umekuwa kitu cha kujivunia na kuonea fahari katika jamii." (uk. 113) .

### 1.0.3 **Mwandishi wa *Upotevu***

Mwandishi wa riwaya ya *Upotevu* ni Mwenda Mbatiah ambaye ni mhadhiri mkuu wa Fasihi ya Kiswahili katika Idara Ya Isimu na Lugha za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Nairobi. Mwandishi huyu amesomea shahada yake ya kwanza katika Chuo Kikuu cha Nairobi kati ya mwaka wa 1985 na 1988 (Bachelor of Arts, B.A. Hons.). Kati ya mwaka wa 1988 na 1990, alisomea shahada yake ya pili (Master of Arts M.A. ) katika sanaa ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Nairobi. Kati ya mwaka 1994—1999, alisomea shahada ya Udaktari katika fasihi, Katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

Baadhi ya vitabu vya kibunifu alivyoandika ni kama:

- *Wimbo mpya* *(2004)*
- *Migogoro* *(2006)*
- *Vipanya vya Maabara* *(2007)*
- *Msururu wa Usaliti* *(2010)*
- *Majira ya Tufani* *(2012)*

Vilevile amehariri mkusanyiko wa hadithi fupi zifuatazo:

- *Mwenda Wazimu na Hadithi Nyingine* *(2000)*
- *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* *(2007)*

Kando na kuwa mhadhiri, Mbatiah ni mwandishi wa kazi za kubuni na pia mhakiki. Kama mhakiki, ameandika vitabu na makala za kitaalamu.

## 1.1.0 TATIZO LA UTAFITI

Utafiti unachunguza dhamira ya uozo katika riwaya ya *Upotevu.* Tatizo hasa ni kuchunguza ni kwa kiasi gani dhamira ya uozo inajitokeza katika riwaya hii. Katika kazi za kifasihi, mtunzi anapoanza utunzi huwa ana ujumbe anaotaka kuuwasilisha kwa wasomaji. Ujumbe huu ni ile jumla ya maana anayoivumbua mwandishi aandikapo na jumla ya maana anayoitambua msomaji katika usomaji wake.

Wamitila (2002:55), anasema kuwa, matukio yanayopatikana katika kazi ya kifasihi, matendo ya wahusika pamoja na mkondo au mfuatano wa matukio hayo vinahusiana kwa kiasi kikubwa na dhamira ya kazi inayohusika. Anasisitiza vilevile kwamba, matukio hayatokei tu bali hutokea kwa kuwa mwandishi anataka kuliendeleza swala fulani au ana nia fulani maalum. Ni kutokana na ukweli huu ambapo tumeteua kuhakiki dhamira ya uozo katika riwaya ya Upotevu ili kubainisha shabaha ya utungo huu wa kifasihi.

## 1.2.0 MADHUMUNI YA UTAFITI

Madhumuni ya utafiti huu ni:

(i) Kuchanganua dhamira ya uozo katika riwaya ya *Upotevu.*

(ii) Kuchunguza uhusika unavyotumiwa kuendeleza uovu.

(iii) Kuonyesha madhara ya uovu katika jamii.

## 1.3.0 SABABU ZA KUCHAGUA MADA HII

Tumechagua kuhakiki riwaya ya *Upotevu* kwa sababu ina udhihirisho wa dhana ya uozo kwa kina kirefu. Waaidha, tumechagua mada hii kwa sababu hakuna mhakiki aliyeshughulikia dhamira ya uozo na athari zake kwa jamii katika riwaya ya *Upotevu.*

Aidha, hakuna mhakiki aliyeshughulikia tatizo la utafiti huu kwa kutumia nadharia tunayoitumia ya Maadili. Vile vile kazi yoyote ya fasihi haikamiliki hadi pale itakosomwa na kutolewa kauli.

## 1.4.0 UPEO NA MIPAKA

Utafiti huu unajikita katika riwaya ya *Upotevu.* Tunahakiki kazi hii ili kubainisha dhamira ya uozo na taathira zake kwa jamii. Kazi hii imeegemea zaidi upande wa maudhui yanayoendeleza uozo.

Pia, utafiti huu ulichunguza wahusika wanaoendeleza dhamira ya uozo. Tunachunguza uhusika kwa sababu tunaamini umechangia katika kubainisha dhamira ya uozo kutokana na mwingiliano uliopo baina ya muundo wa kazi na uendelezaji wa kidhamira.

Hali kadhalika, kazi hii imetathmini athari za uozo huo kwa jamii. Utafiti wetu unamulika kwa jicho pevu madhara ya uovu katika jamii huku riwaya ya *Upotevu* ikiwa kama mizani yetu ya kupimia athari hizo.

Kazi hii haitaingilia swala la matumizi ya lugha. Hata hivyo, tumeirejelea lugha pale ambapo tulihisi inachangia katika kuendeleza uovu. Waaidha, pale ilipobidi, kazi nyingine

za waandishi wengine zimerejelewa na kunukuliwa ili kutilia mkazo maswala ambayo tumeyashughulikia.

## 1.5.0 NADHARIA TETE

Kutokana na malengo tuliyonayo, nadharia tete zetu ni hizi:

(i) Uozo mwingi unaojitokeza katika riwaya ya *Upotevu* una chanzo chake katika malezi mabaya wayapatayo wahusika.

(ii) Wahusika waliosoma ndio wanaoongoza katika kueneza uovu katika jamii.

(iii) Uovu unaleta athari hasi katika jamii.

## 1.6.0 MSINGI WA KINADHARIA

Utafiti huu uliongozwa au ulifanywa katika misingi ya nadharia ya Maadili.

Anapozungumzia uhakiki wa kimaadili, Wamitila (2003:266) anasema kuwa nadharia hii imeasisiwa na mhakiki wa Kiyunani wa zamani, Plato. Mwandishi huyu anafafanua kwamba uhakiki wa kimaadili umetangulia mikabala mingine yoyote ya kihakiki. Nadharia hii imejengeka juu ya imani kuwa fasihi ina wajibu mkubwa kwa jamii. Nadharia hii hutumiwa kuelezea usomaji na tathmini ya kazi ya kifasihi kwa kuangalia uhusiano wake na ubinadamu na haswa masuala ya Kimaadili.

Kutokana na mawazo ya Wamitila (k.h.j), tunapata ufahamu kuwa umuhimu wa fasihi hautokani tu na jinsi ya kusema bali pia katika kile kisemwacho. Wahakiki wanaotetea mtazamo huu huiangalia fasihi kama kitu kinachohakiki maisha ya mwanadamu. Kwa

hivyo, mhakiki anayetumia mkabala huu anatakiwa aone namna ambavyo maandishi yenyewe yanaweza kuwa na funzo au onyo kwa msomaji wake.

Plato katika kitabu chake maarufu *The Republic,* anadai kuwa lengo kuu la fasihi ni kuadili na isipofanya hivyo basi inafaa ipigwe marufuku. Mwanafalsafa huyu, katika kitabu chake hicho, alihusika sana na athari za maadili ya mshairi. Kwa mfano, alishikilia imani kuwa ushairi hauna budi kuchunguzwa kabla ya kupitishwa. Kwa njia hii, inawezekana kuchuja athari za ushairi kwa jamii na hasa watoto na vijana. Waaidha, Plato na wanaozingatia uhakiki huu wanaamini kuwa ushairi hauna budi kumtumikia mtu kiroho, kumnawirisha pamoja na kumpa uadilifu wa kijamii. Kwa njia hii, ushairi huo au utungo wowote wa kifasihi utamwelekeza anayehusika jinsi ya kuwa mwanajamii bora.

Ukweli wa maoni ya Wamitila (2003:266) kuhusu kuiangalia 'fasihi kama kitu kinacho hakiki maisha ya mwanadamu,' unathibitishwa na Wafula na Kimani (2007:24-30), wanaotueleza kwamba Aristotle, ambaye alikuwa mwanafunzi wa Plato, alifahamikiwa na fikra za mwalimu wake. Kwa upande wa fasihi, Aristotle anayarejelea masuala yayo hayo aliyoyazungumzia Plato. Anakubaliana na Plato kwamba fasihi ni sanaa inayoiga mazingira yaliyomzunguka mtu. Aristotle anasisitiza kwamba fasihi haiigi kikasuku; kinyume na hayo fasihi huiga kiubunifu kwa kuzingatia mambo yanayoathiri maisha ya binadamu. Uigaji huu unaweza ukawa wa shari au wa heri. Hivyo basi, jamii inapaswa kuangalia na kuchuja yafaayo kuigwa na kupuuza yasiyofaa. Katika msingi huu, fasihi inakuwa kama kielelezo cha jamii.

Kwa kuegemea katika nadharia ya Maadili, wafuasi hawa wanaamini kuwa fasihi inapasa kuyafichua maovu yaliyopo katika jamii na kuielekeza jamii kwenye mema kwa kubainisha njia za kuushinda uovu. Ndiposa kazi nyingi za fasihi ya Kiswahili zinaelekea kuegemezwa kwenye misingi ya Kimaadili. Hivyo basi, maelezo ya Plato yanatufundisha mafunzo kadhaa. Kwanza, fasihi inatokana na uigaji wa mazingira ya mtu. Pili, fasihi inapaswa kuhakikiwa. Tatu, lengo kuu la fasihi ni kuadili na isipofanya kazi hii ya kuadili, inaweza kupigwa marufuku.

Timmons (2002:64) katika, *Moral Theory: An Introduction*, anasema kwamba kuna aina mbili ya madhumuni muhimu ya nadharia ya Maadili, nayo ni ya kiutendaji na ya kinadharia.

Nadharia ya Maadili ya kiutendaji inahusu utaratibu unaofuatwa ili kutambua jambo lipi ni sawa na lipi si sawa.

Nadharia ya Maadili ya kinadharia inahusu kiini kilichomo katika utendaji ulio sawa na usio sawa. Ubaya na uzuri wa jambo. Kwa hivyo, nadharia hii inalenga kuchanganua kilichomo ndani ya vitendo ambacho huvifanya vitendo hivyo kuwa sawa au kutokuwa sawa.

Maoni haya ya mwandishi huyu kuhusu aina mbili ya madhumuni muhimu ya nadharia ya Maadili yanaelekea kuoana na yale wanayoyasema waandishi walionukuliwa hapo juu, kwamba nadharia hii inajihuhusisha na utaratibu wa kuingilia na kuchunguza kazi za kisanaa katika kuchuja yaliyo mapotovu, na yale yaitwayo maadili katika maisha ya binadamu. Pamoja na hayo, Timmons anaongeza kwamba kila jamii ina kanuni zake ambazo kwazo kitendo chaweza kuonekana sawa au si sawa.

Kuhusu historia, Timmons anasema kwamba wawakilishi maarufu wa nadharia hii ni Plato na Tolstoy, wote walikuwa wataalamu maarufu kutokana na kazi zao nyingi walizoandika. Plato anazungumzia jamhuri dhahania ambayo ni kielelezo bora na yenye kiongozi mwenye maadili ya juu sana. Plato anasema kuwa kiongozi huyu hapaswi kusikiliza muziki wa kuvuta hisia wala kutazama michezo jukwaani ambayo wahusika wake waovu hushinda. Viongozi hawa wanatengwa na uovu huu ili wasije wakapoteza maadili. Plato anapendekeza kuwa watoto ambao wangekuwa viongozi wa jamhuri hii, wangelelewa katika mazingira ambamo hawangeathirika vibaya kimaadili.

Plato alifikiri kuwa suala muhimu zaidi lilikuwa kujali masilahi ya jamhuri nzima isiyokuwa na mtafaruku wala ufisadi kwa sababu mazao ya maovu haya mawili ni kudumaa katika uovu.

Kimani na Chimerah (1999:130) wanaeleza kwamba nadharia ya Maadili inajikita katika imani isemayo kuwa wanadamu, na viumbe wote hai kwa jumla, wana kitu kiitwacho tabia. Kitu hiki hawazaliwi nacho bali hujifunza. Tabia ina pande mbili: mbaya na nzuri. Wanazidi kufafanua kwamba mtu ana uwezo wa kuwa na tabia nzuri iwapo atapata fundi, awali akiwa mtoto mdogo ili afundishwe kutenganisha tabia nzuri na tabia mbaya, ilimradi yeye awe tu na tabia nzuri.

Wataalamu wa nadharia hii wanadahili ya kwamba tabia ndiyo itenganishayo wanadamu na wanyama. Mtu anayeteua tabia mbaya kuwa ndizo zimwongozazo katika maisha huwa hana tofauti na mnyama, hivyo, huitwa hayawani, au hata mnyama. Athari ya maisha ya uovu ina mvuto mkubwa kwa watu wengi.

Nadharia hii inashikilia kwamba, watu wote wanastahili kuwa na tabia nzuri, kwa hivyo, ni wajibu wa kila mtu mwenye tabia nzuri kuwalazimisha hao wenye matendo maovu kayaacha, badala yake, kuwa watu wema, wenye tabia nzuri.

Kwa mtazamo wa nadharia hii, ni wajibu wa waalimu kuwatia adabu wanafunzi wenye tabia mbaya ili waishi kuwa na tabia nzuri. Mtoto mwenye tabia mbaya lazima arudiwe, kwa sababu "mcha mwana, kulia, hulia yeye" Hivyo, jukumu mojawapo la mwalimu ni kuhakikisha kwamba vitendo viovu vinakomeshwa, na uovu unafutiliwa mbali.

Msingi wa nadharia hii unatokana na imani kwamba tabia imejengeka vipande vipande, na kwamba mwenye kuvipanga sawa sawa vipande hivyo, vikaingiana kiasi cha kupatikana kitu kamili na kizima, ndiye mwenye kupata maendeleo duniani. Hivyo, katika lugha kwa mfano, kuna lugha chafu na lugha safi. Upande wa fasihi, kuna fasihi nzuri yenye kufundisha maadili bora na mbaya yenye kupotosha. Fasihi nzuri yapasa ifunzwe shuleni, ilhali watoto hawapasi hata kupesa fasihi mbaya.

Katika mitaala ya elimu, nadharia hii inatekelezwa na wanaelimu wa kihafidhina kama vile Ralph Tyler, na wakurufunzi wake kama Hilda Tabba, raia wa Marekani. Aliyetia fora katika kuisambaza nadharia hii katika uwanja wa elimu ni Bloom (1988), ambaye ni Mmarekani pia. Wanashikilia kwamba anayefunzwa maadili sharti awe mwanagenzi tu. Yeye kubobea katika wema, sharti apitishwe na wataalamu wapevu waliokomaa kumshinda, kwa kuonyesha uhodari wake katika kuyakariri mengi yenye busara yaliyonudhumiwa na waliotambuliwa kuwa watu wenye busara hapo mbeleni. Katika mfumo huu, mtu hufunzika

kwa njia ya kuiga wajuzi wa mambo. Mwanafunzi bora hujifunza kutokana na makosa anayoyafanya mwenyewe kwa kuyaepuka wakati mwingine.

Kwa muhtasari, nadharia ya Maadili inazingatia mambo yafuatayo: Mwanadamu hazaliwi na tabia bali hujifunza tabia mahsusi. Tabia ina pande mbili: nzuri na mbaya. Kukubali maadili ya wakongwe wa fasihi, hasa kuiga tabia za wahusika wema na kuepuka tabia za wahusika waovu. Nadharia hii inaonya pia kuwa athari ya hali ya maisha ya uovu ina mvuto mkubwa sana kwa watu wengi. Waaidha, tabia imejengeka vipande vipande; mwenye kuvipanga vipande hivyo sawa sawa vikaingiana na kuwa kitu kamili ndiye mwenye kupata maendeleo duniani.

Inatuhimiza kujifunza lugha teule iliyotumika na kunukuu kauli takatifu kutoka vitabuni. Umuhimu wa fasihi hautokani tu na namna ya kusema bali pia katika kile kisemwacho. Hivyo, tufanye uteuzi unaostahiki wa vitabu vya fasihi tukufu, pia, tusiwaruhusu wanafunzi kutalii fasihi wapendavyo. Isitoshe, jamii zimulikwazo na fasihi ni nyingi sana, na zinatofautiana pakubwa katika mielemeo ya kiadili. Mwisho, inalenga kuchanganua kilichomo ndani ya vitendo ambacho hivifanya vitendo hivyo kuwa sawa au kutokuwa sawa.

Ni kwa misingi hii ambapo tunahisi kuwa nadharia hii ni bora zaidi kutumika katika kuchunguza mada ya utafiti huu.

## 1.7.0 YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI

Okombo ( 2011 ), ameshughulikia dhamira katika *Utenzi Wa Tambuka*. Mhakiki huyu amebainisha dhamira ya Utenzi huu kama kudhalilisha dini ya kikristo na kuitukuza dini ya kiislamu. Okombo ameonyesha kuwa katika kuiendeleza dhamira, mtunzi amefanya uteuzi

maalum wa sitiara, taashira na tashibiha ili kuunda muumano na muwala wa kisemantiki ambao unalenga kubaini dhamira lengwa. Vile vile, mtunzi wa utenzi huu amewasawiri wahusika wa kiislamu kiubunifu kwa kuwapa sifa zinazoakisi na kuiendeleza dhamira yake. Katika kazi hii ,Okombo pia ametudokezea baadhi ya maudhui yaliyotumika katika uwasilishaji wa dhamira ya *Utenzi Wa Tambuka.* Ingawa uhakiki huu ni wa utenzi, ulitufaa kwa kutoa mchango katika uchanganuzi wetu wa dhamira. Ulitupa miale ya mawazo kuhusu uendelezaji na ukuzaji wa dhamira.

Vilevile, kazi ya Watuha (2011), ilitufaa katika kuyaelewa maswala yanayohusiana na wema na uovu kwa sababu ametumia nadharia ya Maadili katika kuhakiki maudhui ya nyaadhi katika *Utenzi wa Adili* wa Shaaban Robert. Ilitusaidia pia kuyafahamu vilivyo maswala yanayohusiana na nadharia ya Maadili.

Nkonge (2006), amechambua riwaya ya *Nguvu ya Sala* kwa kuyamulika maswala mbalimbali ambayo kazi hiyo inayaibua. Ameangalia maudhui yanayojitokeza katika riwaya hiyo, ambapo swala la uozo wa jamii limejitokeza kama maudhui mojawapo. Ijapokuwa utafiti wa Nkonge ulihusu maudhui, maelezo yake machache kuhusu uozo wa jamii yametusaidia kuelewa habari za kimsingi kuhusu uozo.

Mong'eri (2000:9), akimnukuu Mbughuni (1978:99), anaeleza kuwa kinyume cha maadili ni uovu, ambao una chanzo chake katika ukosefu wa mafunzo. Anasisitiza kuwa Hasidi na Mwivu katika riwaya ya *Adili na Nduguze* wanadhihirisha uovu kwa sababu waliyapuuza mafunzo ya kimaadili na hivyo basi kufanya mioyo yao kudumaa. Wanapopungukiwa na

mafunzo haya wanazidi kuwa wabaya kwa sababu uovu hupata mchango wenye rutuba kwa wale waliokosa ufahamu wa kimaadili.

Hali kadhalika, Mong'eri (k.h.j), anatueleza kuhusu wahusika wanaoendeleza uovu katika riwaya za Shaaban Robert. Kwa mfano katika riwaya ya *Adili na Nduguze,* wahusika wakuu waovu ni Hasidi na Mwivu. Wana wivu, ubinafsi, kiburi, na uchoyo. Tunaambiwa:

> ---- Tabia za Hazidi na Mwivu haziwi tofauti na wanyama. Hawana hata chembe cha utu, ni wazembe, na wamekosa uangalifu katika matumizi ya fedha kwa sababu ya kupenda anasa, wanaaribu mali nyingi walioachiwa na baba yao… (Uk. 44)

Mwandishi Shaaban Robert, hakupenda kuona maovu katika jamii. Matarajio yake yalikuwa kuona jamii yenye usawa, ndiposa katika kazi zake nyingi anapinga kwa ukali mfumo wa kijamii unaokandamiza wanawake, anahimiza kuwa wanawake wanastahili kuvipinga vitendo viovu dhidi yao. Shaaban Robert katika kushughulikia maadili anatumia mbinu ya kiistiara ili kuhimiza maadili fulani, vilevile anatumia mbinu hiyo kubeza tabia fulani potovu. Vilevile, tunaelezwa kwamba Shaaban Robert anakashifu watu wanaoabudu mizimu. Hivyo, wamtambue Mungu na waache ukafiri.

Shaaban Robert, katika nathari zake, anawapa wahusika majina yanayooana na matendo yao maovu kama vile Mwivu, majivuno (kiburi), Fujo, Boramimi. Waziri mkuu wa nchi ya Kufikirika katika nathari ya *kufikirika,* anajitokeza kuwa mwovu, uovu wake unaonekana pale anapotumia kifua kuhalalisha kafara ya binadamu kinyume na ilivyo katiba. Pia katika *Utubora Mkulima,* Makuu anachorwa kama mhusika mwovu – anajitakia makuu. Mhusika Sheha pia ni mpenda pesa. Kazi ya *Siku ya Watenzi Wote* nayo, ina wahusika wadogo walio waovu.

Uhakiki wa Mong'eri ni muhimu katika utafiti wetu kwa sababu unatupanua mawazo na kutupa mwangaza juu ya namna ya kuchunguza dhamira katika kazi za kifasihi; maadam, lengo lake kubwa lilikuwa kuhakiki dhamira ya maadili nasi tunahakiki dhamira ya uovu. Maoni haya, na ya wahakiki wengine tuliowaangalia, yana uhusiano na utafiti wetu, kwa sababu yametajataja baadhi ya mambo tunayoshughulikia katika kazi hii. Tofauti ilioko baina ya maoni yao na yetu ni kuwa, sisi tunashughulikia maudhui ya uovu pamoja na athari zake kwa kina kirefu zaidi.

Hata hivyo wahakiki hawa wametoa uchochezi muhimu katika utafiti wetu unaotufanya kupiga mbizi kufikia mahali ambapo hawakufika.

## 1.8.0 NJIA ZA UTAFITI

Utafiti wetu ulihusu kusoma maktabani. Tulisoma yaliyoandikwa kwenye tovuti kuhusu uozo na dhamira. Tulijifahamisha pia na yaliyomo kwenye mtandao kuhusu nadharia tuliyoitumia ya Maadili. Aidha, tumerejelea maandishi mengine yahusuyo nadharia ya Maadili kama vile tasnifu zilizotumia nadharia hiyo. Maandishi haya yalitufaa katika kuifahamu nadharia hii ya uhakiki wa fasihi na kuweza kuitumia ipasavyo.

Tulihakiki riwaya ya *Upotevu* kwa kuisoma na kuchambua uozo unaowakumba wanajamii na unavyowaathiri, mikakati wanayoitumia kujikomboa kutokana na mitego ya uozo. Tulifanya mahojiano na mtunzi wa riwaya hii na wanafasihi wengine. Tulifanya mahojiano hayo na mtunzi kuweza kutueleza kuhusu maisha yake, uandishi wake, mitazamo yake kuhusu uozo. Wataalamu wengine waliweza kuhojiwa ili kutueleza maoni na mitazamo yao kuhusu mada yetu. Ushauri wao ulitufaa katika kila hatua ya utafiti huu.

# SURA YA PILI

## *DHAMIRA YA UOZO KATIKA RIWAYA YA UPOTEVU*

## 2.0.0 UTANGULIZI

Katika sura hii, tumechunguza dhamira ya uozo katika riwaya ya *Upotevu.* Tumefanya hivyo kwa kumulika maswala mbalimbali yanayoibushwa na kazi hii na ambayo yanaakisi dhamira ya uozo unaotajwa na mwandishi kama upotevu.

Mtunzi wa riwaya ya *Upotevu* anatusimulia kwa kina kirefu matendo ya upotevu anayoyataja kama 'ukware,' huku wenye kutenda matendo hayo wakidai eti huo ndio 'usasa.' Mhusika mkuu ambaye ni Kemathi na wenzake wanangojewa na jamii kuipa mwelekeo kutokana na elimu yao lakini sivyo iwavyo. Mwandishi anajitokeza kushughulikia dhamira ya uovu, yaelekea analenga kutoa onyo pamoja na kutahadharisha jamii dhidi ya uovu.

## 2. 1. 0 UOZO KATIKA JAMII

Jamii ambayo imesawiriwa na mwandishi wa *Upotevu* imepotoka kimaadili. Mwandishi wa riwaya hii amejizatiti katika kuubainisha uozo uliokita mizizi katika jamii yake kwa uwazi na ukamilifu wa kutosha kuweza kumfanya binadamu ajione, ajifunze na kujikosoa. Maovu ambayo tunashuhudia katika jamii husika ni mengi:

### *2.1.1 Ufisadi*

Mwandishi anatanguliza kazi kwa kutudokezea kwamba ufisadi ni kama maradhi yanayoendelea kufyonza uhai wa nchi. Anazidi kueleza kuwa ufisadi huo umesababishwa na sera potovu ambazo hazina kichwa wala miguu (uk. 5). Mwandishi anatuchorea jamii iliyojaa ufisadi kwa sababu ya kutokuweko kwa utaratibu maalum wa kimaadili. Katika jamii hii, kuna wahalifu walioiba mali ya umma, wauaji na wafisadi waliojitajirisha kwa njia haramu. Tunaelezwa kuwa wahalifu hao wanaweza hata kununua uongozi na kuingia bungeni, ilhali wazalendo kama wapiganiaji uhuru, wasomi, kwa mfano Oki – Ojok, na watetezi wa ukweli wanateswa na kunyimwa haki zao.

Oki-Ojok alikuwa ni msomi na mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Nairobi aliyewajibika na kupendwa na wengi. Nguli Kemathi alipojiunga na chuo kikuu, Oki- Ojok alikuwa ametoka na hakubahatika kufunzwa na yeye. Kando na hayo, Oki-Ojok alikuwa mhariri mkuu wa kamati ya uhariri iliyoitwa Shirika la waandishi Kenya- Shiwake. Alimsaidia Kemathi kuhakiki muswada wa hadithi fupi, yaani *Migogoro.* Katika kikao mojawapo cha wawili hao, Oki-Ojok alimweleza Kemathi kwamba:

> "Ukoloni ulipong'olewa," aliendelea, "nilipaza sauti
> Kama mwandishi, msomi na mzalendo. Kwanza
> nikasema kwamba tunapaswa kukomesha uroho
> na ufisadi ulioachwa na wakoloni. ------ unajua
> nilivyoambiwa? Nilikemewa, nikaitwa mchochezi
> na msaliti, kisha nikafungwa kwa miaka kadhaa,

sasa tangu nitoke kizuizini, wameninyima kazi." (Uk. 44)

Hapa, mwandishi anadhamiria kutuonyesha wasomi na wazalendo kama Oki-Ojok ambao baada ya kuyachunguza na kuyaelewa matatizo ya jamii, walijitolea kukemea maradhi ya ufisadi na kuwataka viongozi kubuni sera bora za uongozi. Licha ya kuwa maneno anayoyasema msomi huyu yalibeba ukweli mchungu kwamba nchi yake haikuwa na matumaini ya kupata maendeleo ya kweli kama haikubadilisha mwenendo wake, anatiwa kizuizini. Alipotoka kizuizini, alizidi kuwindwa na askari kanzu, wakitaka kusikia maneno yake ili wamkamate kwa kile walichozoea kukiita "uchochezi."

Mwandishi kupitia kwa Kemathi anatueleza kwamba kiini cha tanzia ya ajali barabarani ni ufisadi. Biashara ya magari ya matatu inajumuisha magari mabovu na yanayoendeshwa ovyo ovyo. Pingu za ufisadi ziliwafunga mikono maafisa waliokuwa na wajibu wa kutekeleza sheria za barabarani. Kuna watu wengi wanaotua mizigo yao ya maisha (kufa) barabarani kwa mfano Motethia , ( kifungua mimba katika familia ya mzee Taramba) na familia yake yote walisagwa katika ajali ya barabarani. Nabea babake Kemathi, pia alihusika katika ajali barabarani na akafa. Mamake Ok-Ojok pia alinusurika kifo baada ya kuhusika katika ajali za namna hiyo.

Aidha, tunaelezwa kuwa mvua kubwa iliweza kugeuza barabara za jiji la Nairobi kuwa mito. Hivi ni kwa sababu mifereji iliyodhamiriwa kuyaondoa maji hayo barabarani ilikuwa imezibika na ilikuwa haipo kabisa. Pesa zilizotengewa shughuli ya kuzibua mifereji hiyo zilikuwa zimeingia mifukoni mwa wasimamizi wa baraza la jiji. Wasimamizi hawa

walitawaliwa na uozo wa ufisadi. Inasemekana pia kuwa wakenya waliojua jinsi ya kutumia pesa kuifunika macho sheria walishajenga nyumba juu ya mifereji hiyo. (uk. 129).

Isitoshe, kuna uozo wa ufisadi ambao unaendelezwa na viongozi. Chifu M'Ngaroni pamoja na wazee wa kijiji ni wafisadi. Baada ya kifo cha babake Kemathi, nduguze, Getonga na Moronge walitaka kujigawia urithi wa baba yao hasa shamba, bila kuwahusisha watoto wengine katika familia yao ambao ni Kemathi, Kagweria na Mbaabu. Tunaelezwa kupitia kwa mhusika Mbaabu kwamba: "Hata wale ng'ombe watatu na punda wameshajigawia wakamuachia mama mbuzi tu." (uk. 131)

Ndugu hao, Getonga na Moronge waliwagawia pesa wazee wa kijiji pamoja na chifu ili wawaunge mkono katika njama zao. Huu ni ufisadi wa moja kwa moja. Inavunja moyo kuona watumishi wa serikali kama chifu wakiunga mkono uovu wa ukiukaji sheria za nchi, na kufanya mapendeleo katika huduma zao kwa umma. Vita vya uhuru vilidhamiria kumaliza maovu kama haya, kumbe sivyo.

### *2.1.2 Dhuluma*

Tunatumia neno dhuluma kwa maana ya maonevu, matendo yasiyo ya haki, ukatili, kudharauliwa, kuvunjiwa heshima na hata kupigwa.

Katika riwaya ya *Upotevu*, dhuluma inaendelezwa na polisi, ambayo ni tabia waliyoirithi kutoka kwa wakoloni. Kuna polisi anayeingia basini na kukosa kulipa nauli kama ilivyo mazoea yao. Tunaelezwa kwamba abiria walipokumbana na tabia hiyo, iliibua hadithi chungu nzima juu ya dhuluma walizofanyiwa na polisi. Kemathi, mmoja wa abiria katika

basi hilo aliwaza kwamba haikuwa haki kuwachukia polisi bila kuelewa kiini cha tabia zao, ni tabia walizorithi kutoka kwa wakoloni. Kisha mwandishi anatubainishia kuwa:

> Chini ya ukolini, polisi hawakuwa watumishi wa umma bali fimbo ya kuwapondea Waafrika. Ukoloni uliitaji fimbo hii kwa sababu ulikuwa wa kimabavu na kiubaguzi wa rangi. Ilikuwa lazima Mwafrika apigwe na kudhalilishwa ili amtii mzungu na kumuogopa. (uk. 9)

Hivyo basi, polisi hawakufunzwa kuwaheshimu raia. Hii ni tabia tunayoiona miongoni mwa polisi hata leo katika jamii tunamoishi. Ndiposa wananchi wengi wanawachukia. Hata hivyo, serikali iliyomo sasa katika nchi yetu ya Kenya inajitahidi kubadilisha hali hii.

Kuna kunyimwa haki pale ambapo Oki –Ojok, mtetezi wa haki anapopinga sera potovu za serikali anatiwa kizuizini (uk. 42). Aidha, hakuna uhuru wa kusema na hata alipotoka kizuizini aliwindwa na askari kanzu wakitaka kuyasikia maneno yake. Kwa hakika ni vigumu sana kwa nchi yenye utawala wa kimabavu kama huu kuendelea pasipo na kuwashirikisha wazalendo katika uundaji sera.

Mwandishi anamsawiri Nabea, babake Kemathi, akiwa mpenda haki, na alitaka mali yake igawanywe miongoni mwa watoto wake kwa usawa na kwa wakati ufaao. Lakini alipokufa, baadhi ya watoto wanawadhulumu wenzao kwa kutaka kujigawia urithi wa baba yao na kuwanyima haki wadogo wao. Pia chifu M'Ngaroni katika huduma zake kwa raia hatekelezi haki. Anaegemea upande wa waliompa rushwa na hivyo kutoa hukumu zisizo za kweli.

Ndiposa Kemathi anamwambia kwamba: "Ikiwa utasaidia watu hawa kutunyanganya mali yetu, basi mambo haya tutayapeleka mahakamani!" (uk. 144)

Baada ya kifo cha Nabea, nduguze Kemathi, Getonga na Moronge walimdharau mama yao kwa kutoshauriana na yeye kwa jambo lolote. Walizama katika mashindano ya kujitajirisha wenyewe. Mbaabu anamweleza Kemathi kupitia kwa barua aliyomwandikia kwamba, jinsi mambo yanavyofanywa nyumbani kwao sasa, ni kama kwamba mama hakuwa hai. Mamake Kemathi alikiri kwamba waliyoyafanya wawili hao hayakuwa ya haki lakini hakuwa na njia ya kuzuia uozo ulioendelezwa nao. Mbaabu pia anasimulia kwamba hawezi kwenda kuwashtaki nduguze kwa chifu kwa sababu chifu M'Ngaroni hatamsikiliza kwa sababu ya ujana wake.

Kulingana na nadharia ya Maadili , msisitizo umo katika kukubali na kuiga tabia za wahusika wema na kuepuka tabia za wahusika waovu. Mzee Nabea alikuwa ni mwenye maadili mema yaliyopaswa kuigwa na watoto wake, ajabu ni kwamba watoto wake wakubwa, yaani Getonga na Moronge wanaishia kuwa na tabia iliyo kinyume na baba yao. Mama yake Kemathi anakiri jambo hili kuwa:

> Ukiwa mzazi, Mungu anaweza kukupa watoto wa aina mbili, unaweza kupewa watoto wema ambao watakupenda na kukutunza katika siku zako za uzee. Lakini pia unaweza kupewa watoto ambao, badala ya kukutunza, wanakuletea udhia siku zako za uzeeni.
> (uk. 139)

### *2.1.3 Anasa*

Tunatumia neno anasa kwa maana ya asherati. Ni hali ya kupenda starehe na raha nyingi za mwili kama vile kujitosa katika mapenzi ya kiholela, umalaya, uzinzi, ukware, densi pamoja na tafrija. Anasa ni uovu mojawapo uliotumiwa na mwandishi kuendeleza dhamira ya uozo. Kwa mujibu wa Mlacha na Madumulla (1996:10), mtunzi wa riwaya huwasawiri wahusika na kuwaweka katika mazingira maalum, na kuwazulia migogoro inayoendeleza visa na vitushi vinavyooana katika kujenga dhamira. Katika kuiendeleza dhamira ya uozo katika jamii, mwandishi wa riwaya ya *Upotevu*, amewasawiri wahusika wengi kama wapenda anasa na walionaswa katika mtego wa mitindo ya maisha waliyoiiga bila kuielewa vizuri.

Jamii ambayo inasawiriwa na mwandishi wa *Upotevu* imepotoka kimaadili. Mara nyingi Kemathi alichekwa na rafikize kwa kutoshiriki katika ulevi, jambo ambalo lilimkumbusha jinsi wanakijiji walivyomcheka marehemu babake kwa kutoshiriki anasa mbalimbali. Mapato yake yaliishia katika ulipaji wa karo za shule za wanawe.

Mwandishi anatuarifu kwamba funzo moja muhimu alilolipata Kemathi kutokana na babake ni jinsi ya kulikabili shinikizo la kutii hirimu, marafiki na majirani. Aliamini kuwa mtu mzima alipaswa kujitegemea kimawazo badala ya kuvutwa na hirimu kama mbuzi aliyefungwa kamba. Mahusiano ya mawazo haya na nadharia yetu ya Maadili ni kwamba mwanadamu hazaliwi na tabia bali hujifunza. Tabia ina pande mbili: nzuri na mbaya. Binadamu yeyote ana uwezo wa kujifunza tabia ama nzuri au mbaya. Kwa hivyo, tunaafikiana na imani ya Kemathi aliyoipata kwa babake kuwa mtu mzima anapaswa kujitegemea kimawazo badala ya kuvutwa na hirimu kama mbuzi aliyefungwa kamba.

Jamii anayotuchorea mwandishi ni yenye vijana walionaswa katika mitindo ya maisha potovu. Mhusika kwa jina Chabare ambaye ni msomi na ana digrii kutoka Chuo Kikuu cha Nairobi ni mpenda anasa na hasa wanawake. Katika maisha yake, amali muhimu zaidi ilikuwa ni kuwawinda warembo. Mwandishi anatueleza kwamba Chabare alikuwa na sura yenye mvuto mkubwa kwa wanawake na aliitumia kama ulimbo wa kuwategea. Aliwapata wengi, lakini uchu wake haukutosheka.

Chabare alijitahidi sana kuwatafuta wasichana na kuwatumilia mapato yake yote. Alikuwa na msichana rafiki yake aliyeitwa Flora, mwanafunzi katika Chuo cha Ualimu. Wanapokutana, wanapanga kuhudhuria tafrija ya densi iliyoandaliwa na bendi moja maarufu kutoka Tanzania na wanamtaka Kemathi atafute mrembo kisha aandamane nao. Walimtaka pia Muthomi ambaye ni rafiki yao mwingine ahudhurie. Tafrija yenyewe ingefanyika huko Ndototamu, kilabu maarufu na cha fahari. Kila aliyeingia kwenye kilabu hiyo alikaribishwa na harufu nzuri ya manukato iliyojaa hewani. Tunaelezwa kwamba:

> Asili ya harufu hiyo ilikuwa ni wasichana warembo waliojiegemeza kwenye kuta, wakijaribu kuwavutia wanaume ambao walikuwa wanaingia. Matineja hao watanashati walijulikana kama 'ndogondogo' kutokana na ujana wao na udogo wa miili yao. Baadhi yao walikuwa na bahati, wakapata wanaume ambao waliwachukua kwenda kuwatumbuiza. (uk. 57)

Dondoo hili linatuthibitishia kwamba jamii ya Kemathi ilikuwa ni yenye kupenda na kushiriki katika raha za aina aina huku vijana na wazee wakihusishwa. Kwenye tafrija, ndogondogo walidensi na kuchezesha vifua, huku madodo yao yakitikisika mfululizo na kuwasisimua wanaume ambao walikuwa wakicheza nao. Huu ni uozo unaotuelekeza kwenye utovu wa maadili. Wazee ambao wanatazamiwa na jamii wawe vielelezo bora kwa vijana pamoja na watoto wao, ndio wanaoshiriki anasa na ndogondogo bila kujali familia zao, ni mfano wa jamii iliyooza kwa kukosa uadilifu.

Mbaabu, ndugu mdogo wa Kemathi, alijihusisha na mapenzi badala ya masomo. Siku moja wakiwa nyumbani, Kemathi aliufungua mkoba wa nduguye na kupata barua za mapenzi; thibitisho kwamba akili yake ilikuwa imetekwa nyara na wasichana.

Pamela kagendo, na Flora walisomea katika chuo kimoja cha mafunzo ya ualimu. Pamela Alimsimulia Kemathi habari za Flora kuhusu tabia yake walipokuwa shuleni, anasema kuwa Flora ni mtu wa ajabu:

> Flora ameharibika kabisa kitabia tangu zamani, sijui kama majarida ya *pornography* anayopenda kuyasoma ndio yaliompotosha hivyo; mbali na kuwa kigeugeu na mwenye dharau, Flora ana tabia za malaya. Mambo aliyokuwa akiyafanya tukiwa chuoni hayanenekí! (Uk. 77)

Flora ingawa ana urafiki na Chabare ana wapenzi wengi kando na Chabare. Keremi ambaye ni ndugu yake Chabare, alielezwa na rafiki yake kwamba alimwona Flora wakiingia katika

nyumba ya ofisa mmoja kutoka Murang'a , huku wamezungushiana mikono kwenye viuno vyao. Wakati huohuo, Keremi alirudi nyumbani walimoishi na Chabare kuchukua fulana yake kwa kuhisi baridi. Alipofika nyumbani, alipata mlango umekomewa kwa ndani. Mlango ulipofunguliwa, alimpata Chabare akiwa kitandani na mwanamke aliyemtambua kuwa mtumishi wa nyumbani wa jirani yao. Kisadfa, Flora anarudi nyumbani wakati huo na kumkuta Chabare akiwa na mpenzi huyo mwingine. Swala ambalo lilizua ugomvi mkubwa, huku kila mmoja akimlaumu mwenzake kwa kutokuwa mwaminifu. Ugomvi huu ulimfanya Flora kujiua siku iliyofuata.

Keremi alipomweleza rafiki yake Koome aliyoyakuta nyumbani, alicheka na akasema kwamba: "Ukware sasa ulishapewa hadhi ya digrii ya chuo kikuu. Ukware ulishakuwa kitu cha kujivunia na kuonea fahari katika jamii." (Uk. 113)

Kutokana na matukio hayo ni dhahiri kuwa Flora na Chabare wana uozo wa kitabia uliokithiri. Kemathi ambaye ni rafiki wa Chabare kwa miaka mingi, alishangazwa na vituko vya Chabare, hasa mapenzi. Alipomuuliza Keremi chanzo cha tabia ya ndugu yake, anamjibu kwamba: "Ayafanyayo Chabare ni yale ambayo amekwishajidanganya kuwa ni usasa." (uk. 115)

Katika jamii hii iliyozama katika uozo uliopevuka, tunaarifiwa na mwandishi kwamba ushugadadi, ushugamami, ukahaba na uzinifu ni mambo ya kawaida na ni kama ugonjwa ambao hauna tiba. Isitoshe, kule alikosomea Kagweria dadake Kemathi, baa la ukahaba liliwanasa baadhi ya wasichana, jambo ambalo lilikuwa ni hatari katika enzi hii ya ukimwi.

Ama kweli ni jamii iliyooza na kuozeana ikiwa uovu wote huo unatajwa kama mambo ya kawaida.

Mwandishi ameiendeleza kwa kina kirefu dhamira ya uozo kupitia kwa vitendo viovu vya wahusika kama vile Chabare na Flora ambao wanalingana kitabia. Si hao tu, tunaambiwa kwamba mienendo ya upotovu imeenea sana siku hizi. Muthomi anamwambia Kemathi kwamba:

> Ukware, upurukusheni na upendeleo wa mitindo mibovu ya tamaduni za kigeni ni udhaifu wa kitabia ambao haukuwasibu Chabare na Flora tu, bali umewaathiri watu wote wenye elimu ya wastani. Walioathirika, waliooza zaidi, ni wale waliopata elimu ya juu. Nadhani hivi ni kwa sababu elimu ya juu ndio hasa *hotline* ya kuwasilishia uchafu wote wa utamaduni wa kimagharibi, kutoka huko kwenye asili yake hadi hapa. Sisi ndio majalala ya uchafu huo. (Uk.72).

Kemathi aliyaona maneno ya Muthomi kuwa ni ukweli mtupu kwa kukiri kwamba kizazi chao ni kizazi kilichopotea njia.

Jamii ya Upotevu inakwenda kinyume na inavyodai nadharia ya Maadili kwamba, watu wote wanastahili kuwa na tabia nzuri, na ni wajibu wa kila mtu mwenye tabia nzuri kuwalazimisha hao wenye matendo maovu kuyaacha, badala yake, kuwa watu wema, wenye

tabia nzuri. Wanajamii wengi hapa wanadhihirisha uozo mwingi wa kitabia unaohusisha vijana kwa wazee. Hivyo, vijana hawana vielelezo wala waelekezi.

Wingi wa maovu katika jamii ni jambo la kutamausha. Lakini wa kulaumiwa ni nani? Malezi wayapatayo, elimu, mfumo duni wa uchumi pamoja na utawala mbaya ndio unaochangia katika uozo wote huu.

### *2.1.4 Ukoloni na Ukoloni Mamboleo*

Riwaya ya *Upotevu* iliandikwa miaka mingi baada ya ukoloni lakini bado inadhihirisha chembechembe za maovu yaliyo na mizizi yake katika athari za ukoloni. Kulingana na Mong'eri (2000), "nyakati za enzi ya ukoloni, wale walioelimika, kama vile Shaaban Robert walijitwika jukumu la kupigania haki za kisiasa. Walipinga siasa za dhuluma na kudai mabadiliko katika uongozi wa kisiasa."

Shaaban Robert ni mmoja wa wale waliotumia kipawa cha uandishi wa kazi za kifasihi kupigania haki za kisiasa katika jamii yake ya Tanzania. Jambo aliloliendesha kwa uangalifu bila kushambulia serikali ya kikoloni kwa njia ya moja kwa moja. Kupitia kwa kazi zake za kinathari, kwa mfano kazi ya *Kusadikika* , Shaaban Robert anahimiza mabadiliko ya kisiasa. Serikali ya kikoloni inashauriwa juu ya haja ya kugeuza maongozi yake ya kisiasa yenye dhuluma na kusambaza siasa zenye maadili.

Serikali ya kikoloni iliwatendea waafrika maovu kwa kutumia mabavu na vitisho kama njia ya kufanya raia wake kutenda mambo. Raia hawakutendewa haki na demokrasia

ilikosekana. Viongozi wa serikali hii walikuwa ni wenye tamaa za kibinafsi na uroho waliotaka kujitajirisha wenyewe.

Serikali za kimabavu hazikukubali mawazo mapya hata ingawa mawazo hayo yaliiletea jamii maendeleo. Wazo jipya katika uongozi usiojali maslahi ya wengi huchukuliwa kuwa ni uzushi na ukiukaji wa sheria. Mhusika Oki – Ojok katika riwaya ya *Upotevu* ni mwandishi, msomi na mzalendo. Ukoloni ulipong'olewa, alipaza sauti na kusema kwamba nchi ilipaswa kukomesha uroho na ufisadi ulioachwa na wakoloni. Pili, alishauri kwamba mbinu za kimabavu na kinyapara zilizotumiwa na mkoloni hazingetufaa na zilipaswa kubadilishwa. Ushauri huu alioutoa ulimfanya kukemewa, akaitwa mchochezi na msaliti kisha akafungwa. Ndivyo zilivyokuwa serikali za kikoloni kwamba wazalendo walipigwa kikumbo na kutishwa ili sauti zao zisiufungue umma macho.

Viongozi wa aina hii waliowadhulumu wananchi wao ni waovu na watovu wa maadili kwa sababu hawawashirikishi raia katika uongozi, na wako imara kutupilia mbali mchango wa aina yoyote wa raia unaokusudiwa kuleta maendeleo katika nchi.

Kutokana na uongozi wa sampuli hii, tunaweza kung'amua kuwa chanzo cha upotevu ni migogoro iliyo na mizizi yake katika ukoloni na ukoloni mamboleo. Majilio ya wakoloni yaliteketeza tamaduni za watu weusi, na baada ya ukoloni, watu weusi walishindwa kubuni njia sifaazo za kuendeleza shughuli zao. Hivyo, matokeo yake yakawa ni hii hali ya kupotea njia. Ni kweli pia kwamba waliotawala jana kama wakoloni wakongwe wanaendelea kutawala leo kama wakoloni mamboleo, jambo linalothibitisha ukweli kwamba: "Hadithi yetu ya uongozi tangu uhuru ni tanzia tupu." (uk. 43)

Kupitia kwa mhusika Oki- Ojok, mwandishi anawahimiza wananchi kutia bidii katika kuzipindua sheria zilizopendelea wakoloni na kuwanyima raia haki zao za kimsingi. Oki-Ojok anasema kwamba yeye akiwa ni mwandishi na msomi, ana jukumu la mwaguzi wa jamii yake. Hali kadhalika, aliwajibika kuzifasiri ndoto za kitaifa kwa manufaa ya umma. Vile vile alimwona Kemathi kama kijana aliyeelekea kupata sifa za mwaguzi kama yeye kutokana na kazi alizoandika na kumpa kuhariri.

Utafiti wetu unafanywa katika misingi ya nadharia ya Maadili. Nadharia hii inashauri kwamba mwenye kubobea katika uadilifu, sharti aongozwe na walio waadilifu. Naye mwenye kushauriwa lazima awe tiyari kuyaenzi mengi yenye busara yaliyonudhuliwa na waliotambuliwa kuwa wenye busara. Nadharia hii inazidi kubainisha kuwa mtu hufunzika kwa njia ya kuiga wajuzi wa mambo. Kwa maoni yetu, inaelekea, msimamo wa mwandishi katika kazi hii yake ya riwaya ni kwamba, hakuna maendeleo yenye maana yawezayo kuwepo ikiwa kila raia hatashirikishwa. Mwandishi anawashauri viongozi wawe radhi kupokea mawazo mapya ili taifa lolote liweze kupiga hatua kimaendeleo.

### *2.1.5 Wivu*

Wivu kulingana na Mdee et al (2011), ni hali ya kuwa na kinyongo au kijicho wakati mtu aonapo mali, mafanikio au maendeleo ya mtu mwingine. Ni hali ya kuonea mtu mwingine ubaya kutokana na uwezo wake ambao unaweza kuzidi wako. Wivu ni tabia inayopaswa kupigwa vita katika jamii kwa sababu inarudisha maendeleo nyuma. Ndugu wakubwa wawili wa Kemathi, Getonga na Moronge wana wivu. Kemathi anapobaki mjini kusoma wakati wengine wako nyumbani Desemba, wanadai kwamba huko ni kujisingizia masomo na

kujificha mjini ili kuponda raha za Nairobi. Katika mazungumzo kati ya Mbaabu na Kemathi tunaelezwa:

> --------- Mbaabu aliendelea.
>
> Kemathi alishtuka. "wanafanya hivyo kwa nini?"
>
> "Wivu."
>
> "Wivu? Wivu wa nini?"
>
> "Ah, si unajua kwamba umesoma zaidi kuliko wao?"
>
> "Kweli ---------- eh?" Kemathi alizidi kushangaa. (uk. 17)

Dondoo hili ni dhihirisho tosha kwamba kaka zake Kemathi walimwonea wivu kwa sababu ya kisomo chake. Pia Kemathi alipotaka kuendeleza masomo yake katika chuo kikuu, walipinga na kutofurahia jambo hilo na kukataa kumlipia karo baada ya digrii yake ya kwanza.

Tunaambiwa kuwa marehemu Nabea alikuwa na watoto watano na wote walikuwa hodari shuleni na waliweza kupata kazi baada ya masomo yao. Ajabu ni kwamba wanakijiji walimwonea mzee Nabea wivu kwa sababu ya fanikio hilo. Mara nyingi watu husahau kwamba mafanikio hayajileti yenyewe. Yanatokana na bidii pamoja na kujitolea, kama walivyofanya watoto wa Nabea. Wenye kufanikiwa maishani ni wenye roho safi wanaowatakia wenzao mema na ufanisi kama inavyodai nadharia yetu ya Maadili.

## 2.1.6 Ulevi

Katika tasnifu hii, tunatumia neno ulevi kwa maana pana kujumlisha unywaji pombe, utumiaji wa dawa za kulevya pamoja na vitu vingine vinavyolewesha.

Mara nyingi chanzo cha maovu mengi katika jamii ni ulevi. Katika riwaya ya *Upotevu,* ulevi umesawiriwa kwa kina na wanaohusishwa na ulevi huo wanaonekana kulemewa na uozo wa aina tofauti tofauti. Mtego wa ulevi hauna ubaguzi kati ya wasomi na wasio wasomi, tajiri na maskini. Unawanasa wote kwa pamoja huku wasomi wakiuzamia zaidi.

Katika mtaa wa Dandora anakoishi Kemathi, ana jirani mwanamume ambaye alikuwa amelala hata baada ya kila mtu kuamka. Mbaabu anapouliza kwa nini iwe hivyo? Anaambiwa kuwa alikesha katika vilabu vya pombe. Eti: "---- Ni mwanamume vivi hivi tu, bwege. Ulevi wa kupindukia ulikwisha kumlemeza." (uk. 21)

Aidha, mwandishi kupitia kwa kinywa cha Kemathi anatusimulia kwamba aliona vijana wasiokuwa na walezi wakiangamizwa na dawa za kulevya na pombe duni. Katika jamii hii, kuna watu wanaojitajirisha kwa njia haramu za uuzaji dawa za kulevya . Hii ni ithibati kwamba ni jamii iliyokosa mwelekeo na kupotea ikiwa biashara ni kusambaza ulevi. Serikali haionekani kuwa na juhudi zozote za kukomesha maovu hayo.

Hali kadhalika, katika chuo kikuu, wakati Kemathi anasomea shahada yake ya kwanza, anasimulia kwamba kila walipoyapokea marupurupu yao waliyoyaita *boom* walikwenda ngamani kujiburudisha. Kulikuwa na chakula na vinywaji vya kila aina vikiwemo vileo. Katika maeneo haya, bendi za muziki zililetwa kuwatumbuiza. Mwandishi anatuarifu

kwamba: "Msimu mfupi wa *boom* ulipoanza, marafiki wa Kemathi kama Muthomi na Chabare walichapa maji mpaka asubuhi." (uk. 46)

Kemathi alishangazwa na tabia za ulevi wa kupindukia wa rafiki zake na kukosa kuelewa jinsi walivyoweza kudurusu hata baada ya kunywa vileo. Kwa upande mwingine, Muthomi na Chabare walimcheka kwa "kutojua raha za pombe" ni jambo la kutamausha kwamba pesa ambazo zingetumika katika kujiendeleza na kuiendeleza nchi zinaishia kwa vileo na maovu mengine.

Waaidha, kuna ithibati nyingine ya ulevi inayodhihirika wakati ambapo Ngotho babake Flora, alipewa fursa ya kuzungumza. Ngotho akiwa nyumbani kwa Chabare kujaribu kuchanga pesa za kulipa bili ya Flora ya hospitali, anazungumza huku matamshi yake yakisindikizwa na harufu kali ya pombe. Keremi, ndugu yake Chabare, anapenda sana mambo ya unywaji pombe. Akiwa na rafiki yake Koome, mwanajeshi, walipenda kunywa pombe mpaka hata saa tatu usiku.

Isitoshe, mazungumzo kati ya Kemathi na dada yake Kagweria yanatubainishia kuwa ukosefu wa ajira uliwapelekea vijana wengi kuuendeleza uozo wa kila aina. Waliokosa kazi baada ya kumaliza kidato cha nne, walifungika kwenye uhalifu, matumizi ya dawa za kulevya na ulevi wa pombe, mambo ambayo yaliibomoa miili yao kama ukuta wa udongo ulionyeshewa. Mbaabu naye anaporejea nyumbani saa mbili unusu siku ya Krismasi, amelewa na anazungumza kwa kuburura maneno. Nchi itaendelezwa namna gani ikiwa hata vijana wadogo kama hawa ambao ni tegemeo la kesho wananaswa na ulevi?

### 2.1.7 Tamaa

Tamaa na ubinafsi ni aina nyingine ya uozo ambao unafaa kukemewa katika jamii. Katika Biblia takatifu (1 Timotheo 6:10) tunaambiwa kuwa chanzo cha maovu yote duniani ni kupenda pesa au tamaa ya pesa. Ingawa wakoloni walikuja barani Afrika kuanzia karne ya kumi na tisa na kuendelea kwa madai ya kuleta elimu pamoja na kusambaza dini, nia yao ya kimsingi ilikuwa ni kupora malighafi na kujitajirisha wenyewe, kwa hivyo waliongozwa na uroho pamoja na tamaa ya pesa. Tamaa ya namna hii iliwalazimu kubuni sera za uongozi ambazo zingewafaa katika kufikia malengo yao. Miongoni mwa sera hizi ni kama vile kuwapa Waafrika elimu duni, dini iliyowafunza Waafrika kutii na kunyenyekea, sera za kuleta utengano, utabaka n.k.

Mwandishi wa riwaya ya *Upotevu* anasimulia kwamba ukoloni ulipong'olewa, uroho haukukomeshwa. Walio uongozini sasa hawatofautiani na waliotawala awali. Tunaambiwa kwamba katika chuo kikuu ambako Oki – Ojok ni mhadhiri, tamaa ya pesa inaelekea kuvuruga taaluma ya uhadhiri.

Aidha, Flora alipokufa, hakuna aliyekuwa tayari kulipa deni lililodaiwa na hospitali. Kulizuka ugomvi mkali kati ya Chabare na jamaa ya Ngotho, babake Flora. Mwandishi anasisitiza kwamba kiini cha ugomvi huo hakikuwa kingine bali pesa. Anasema:

> Aliyekufa hakuwa chochote tena machoni mwa babake, nduguye, na mpenzi wake, kitu ambacho kilikuwa cha thamani zaidi ni pesa. Pesa zilikwisha chukua nafasi ya mbele katika jamii hii iliyopotea njia. (uk. 106)

Katika dondoo hili, kuna ukweli usiopingika kwamba pesa na uroho ni kama pande mbili za sarafu moja. Nguvu zake ndizo zilizokifunga macho na kukipotosha kizazi anachokizungumzia mwandishi. Maovu haya yamekifanya kizazi hiki kupeperuka holela ulimwenguni kama chombo kinachoelea baharini bila rubani.

Babake Kemathi alipoaga, nduguze wakubwa, Moronge na Getonga, wanaongozwa na tamaa na wako katika hekaheka za kushindania utajiri. Wanataka kujigawia urithi wa baba yao, hasa shamba bila kuwahusisha watoto wengine wa familia hiyo. Huu ni ubinafsi wa moja kwa moja unaodhihirisha tabia ya kutojali maslahi ya wengine.

### 2.1.8 Elimu na Utamaduni

Wamitila (2003:330) anaeleza maana ya utamaduni kama uzoefu wa kimaisha wa watu fulani. Ni dhana inayoleta pamoja michakato ya kijamii ambayo huiwezesha jamii hiyo kujielezea na kujitambulisha pamoja na kufanya shughuli za kila siku. Kutokana na fasili hiyo, tunaweza kufungamanisha elimu na utamaduni wa watu fulani. yaani, elimu kama mfumo wa mafunzo yanayopatikana maishani, inaweza kuchukuliwa kama sehemu ya utamaduni wa jamii fulani. Mwandishi wa riwaya ya *Upotevu* anazungumzia maswala ya elimu na utamaduni katika kazi zake nyingi, na hasa katika riwaya ya *Upotevu.* Huenda anafanya hivi kwa sababu ya kubainisha umuhimu na nafasi ya elimu na utamaduni katika jamii.

Kabla ya majilio ya wakoloni, Waafrika walikuwa na elimu yao. Vijana walipokea mafunzo kutoka kwa wazazi. Baada ya kuja kwa wakoloni, mambo yalibadilika kwa sababu ya elimu ya Magharibi iliyoanzishwa iliwafunza vijana kuwa ni machache mno ambayo wangejifunza

kutoka kwa wazazi. Malengo ya elimu ya Magharibi yalikuwa tofauti kabisa na yale ya elimu ya Waafrika. Elimu ya Waafrika ilikusudia kumtayarisha aliyeipitia ili aweze kufaa jamii kulingana na mazingira na mahitaji mbalimbali. Kwa upande mwingine, wakoloni walikuwa na nia yao ya kuwaondoa Waafrika katika misingi ya kitamaduni ili kufuata na pia kutumikia utamaduni wa kigeni.

Mwandishi wa riwaya ya *Upotevu* anatuonyesha kuwa elimu iliwatenganisha wazee na vizazi vilivyofuata. Kwa vijana, wazee hawakuwa na nafasi katika ulimwengu uliojaa elimu na utamaduni wa kigeni. Tunashuhudia ukweli huu wakati Flora amefunga shule, anakataa kwenda nyumbani. Anakwenda mjini kukaa na rafiki yake Chabare huku akiwa amemdanganya babake kwamba anakwenda Mombasa kwa dadake. (uk.51)

Wawili hawa wakiwa katika starehe zao mjini, Chabare anamwambia Flora hivi:

> Mimi nimekwambia mara nyingi kwamba
> hawa wazee wetu ni mafala sana, sasa
> babako anataka ukae nyumbani kwa likizo
> ya mwezi mzima ukifanya nini? (Uk. 51)

Flora alivutiwa na maisha ya jiji la Nairobi. Jambo hili lilimfanya ayachukie maisha ya mashambani. Alipenda sana densi, na mara nyingi alilalamika kwamba kwao hapana majumba mazuri ya disko na bendi nzuri. Inaelekea mwandishi anadhamiria kutuonyesha kwamba wasomi waliokengeushwa na elimu ya Magharibi kama vile Chabare na Flora hawawezi kuwa ruwaza ya kuigwa katika jamii. Yale wanayotenda ni maovu yaliyooza na

kuozeana. Licha ya kisomo chake, Chabare anakosa uaminifu na ana tabia ya uzinzi. Flora ni vivyo hivyo.

Mwandishi anamsawiri Kemathi kama kijana aliyependa masomo. Alikuwa ameamua kufuata ndoto ya kupaa katika anga ya elimu. Licha ya ukweli huu, Kemathi alipata pingamizi nyingi katika juhudi za kuendeleza masomo yake. Baada ya shahada yake ya kwanza, kaka zake wawili walipinga hatua ya kuendelea kwake na masomo. Kinyume na Kemathi, Mbaabu hakuzingatia masomo. Alipenda mambo ya wasichana. Maovu mengine ambayo yalikwaza hatua za kuendeleza masomo ni kama vile, ulevi, mimba ya mapema na mila potovu kama vile, imani kuwa, "kumuelimisha msichana ni bure"

Umaskini pia ulikuwa ni kikwazo mojawapo katika kuendeleza elimu, Mzee Nabea alitatizika katika kupata hela za kutosha za kuwaelimisha wanawe. Ndiposa wakati mwingine Kemathi alilazimika kutoa marupurupu yake kuchangia karo wakati ambapo mibuni haikuleta mazao mema. Ndung'u naye alikwenda shule hadi darasa la saba tu, ndio maana Kiswahili chake ni chenye matatizo mengi na kimesongwa na Kikikuyu.

Miongoni mwa sababu zingine, mwandishi anamulika maswala ya upotovu kama yenye chanzo chake katika kupendelea mitindo mibovu ya tamaduni za kigeni. Huu ni uovu ambao haukuwanasa Chabare na Flora tu, bali uliathiri watu wote wenye elimu ya wastani. Isitoshe, mwandishi anashangazwa kwamba waliooza zaidi ni wale waliopata elimu ya juu.

Bila shaka, mwandishi ametamauka kwa kuona kuwa wasomi ambao wangeleta maendeleo katika jamii na hivyo kuinua hali ya maisha wanaipeleka jamii yao katika maafa. Kizazi cha

upotevu hiki kitakombolewa na nani? Linalovunja moyo zaidi ni ukweli kuwa hakuna matumaini ya kuutibu ugonjwa wa ukware ambao umewaathiri wengi.

## 2.2.0 HITIMISHO

Katika sura hii, tumechunguza dhamira ya uozo katika riwaya ya *Upotevu*. Tumeona kuwa jamii ambayo imesawiriwa na mwandishi wa *Upotevu* imepotoka kimaadili. Maovu ambayo tunashuhudia katika jamii husika ni mengi kuliko vitendo vya uadilifu. Swala la uozo katika jamii limechukua nafasi kubwa katika riwaya hii. Uozo pia umesimbwa na mtunzi kwenye kichwa cha riwaya yenyewe. Mwandishi anaonyesha wazi kwamba kizazi chenye kutawaliwa na uovu ni kizazi kilichopotea njia. Mtego wa uozo unaonekana kuwanasa watu wenye elimu ya wastani. Waaidha, waliosoma zaidi hawakuachwa nyuma, ndio waliooza zaidi.

Kupitia kwa wahusika wake, Mwandishi ameonyesha taswira nzuri ya fadhaa inayotawala katika jamii zetu kwa sababu ya kutokuweko kwa utaratibu maalum wa kimaadili. Upotovu wa maadili unaletwa na sera potovu, umaskini, uteketezaji wa tamaduni za watu weusi na wakoloni, upendeleo wa mitindo mibovu ya nchi za Magharibi hasa miongoni mwa vijana, mfumo duni wa uchumi, uongozi mbaya, ukosefu wa utu, ukosefu wa vielelezo bora katika jamii husika, na kadhalika. Kwa maoni yetu, yaelekea mwandishi alikerwa na hali hii ya kuteketea kwa kizazi ambacho ni tegemeo la kesho. Ndiposa anachukua jukumu la kutahadharisha jamii dhidi ya uovu kupitia uandishi wa riwaya hii.

# SURA YA TATU

## UHUSIKA ULIVYOTUMIWA KUENDELEZA UOVU

### 3.0.0 UTANGULIZI

Katika sura hii, tunadhamiria kuonyesha namna ambavyo mwandishi wa riwaya ya *Upotevu* amewasawiri wahusika wake katika kuendeleza dhamira ya uozo. Usawiri wa wahusika ni namna ambavyo wahusika wa kifasihi huwasilishwa na msanii wa kazi fulani. Katika kazi za kifasihi, wahusika hutumika kubeba ujumbe wa mwandishi . Wahusika hao huwa na sifa za kimaadili, kitabia, kiitikadi, na za kifalsafa ambazo hutambulishwa na wanayoyasema, wanayoyatenda, au kupitia kwa maelezo ya mhusika ama msimulizi.

Kimani na Chimerah (1999:250) wanaueleza uhusika kama umithilishaji wa vitendo vya viunde wa hadithini na vile vya viumbe katika ulimwengu razini. Vitendo vya viunde hao husababishwa na kuingiliana kwao na mazingira ya ubunifu, kama ambavyo vitendo vya viumbe razini huwa vinasababishwa na maingiliano baina yao wao wenyewe na mazingira yao, ambayo ni razini. Wanatufafanulia zaidi kuwa vitendo vya wanaohusika katika kutenda vinaweza kuitwa vitendo tu pale utendaji wa viunde ama viumbe unapoleta mabadiliko ya aina fulani katika mazingira na katika tabia za hao wenye kuhusika.

Mabadiliko hivyo basi, ni lazima yasababishwe na miili ya wahusika ikiongozwa na akili, na mnyambuliko ama mfumko wa dhana na mawazo yanayopitikia katika bongo zao. Katika riwaya, usimulizi humsaidia msomaji kuuelewa uhusika na wahusika kama ulivyodhamiriwa na mwandishi.

Wamitila (2003: 123) anamweleza mhusika kama kiumbe anayepatikana katika kazi ya kifasihi na ambaye anafanana na binadamu kwa kiasi fulani. Wasifu wa mhusika unategemea mkabala uliopo. Tunaweza kupanua mawazo haya kwa kusema kuwa; uhusika ni utaratibu wa kuwaumba wahusika pamoja na kunga zinazokwenda na utaratibu huo, hasa utofautishaji na ukuzaji wao. Mhusika ni kiumbe wa kisanaa ambaye ameumbwa makusudi kutekeleza majukumu fulani ya kisanaa anayodhamiria mwandishi. Matendo ya mhusika huyu, mienendo yake, furaha yake, machukizo yake, uhai na ufu wake vinadhibitiwa kwa kiasi kikubwa na dhamira na lengo la mwandishi.

Kwa jumla riwaya ya *Upotevu* ina wahusika wa aina mbili; waovu na waadilifu. Tunapolinganisha idadi ya wahusika wema na waovu, ile ya wahusika waovu inazidi. Hili ni dhihirisho kwamba jamii inayosawiriwa na mwandishi ni jamii potevu, kama inavyoashiria anwani ya kitabu.

Wamitila (2002:54), anasema; Usawiri wa wahusika: wasifu wao, tabia zao, itikadi zao, vionjo vyao na hata mitazamo yao huathiriwa kwa kiasi kikubwa na dhamira ya kazi fulani. Katika msingi huu tunachunguza uhusika ulivyotumika kuendeleza dhamira ya uozo. Uovu hudhihirika katika lugha waitumiayo wahusika, dhima au majukumu waliyopewa, muundo na msuko, mtazamo, maudhui, mwonoulimwengu na uhamasishaji.

*Lugha* ndiyo inayotumika kama chombo katika kuiunda kazi yoyote ya kifasihi na kuwajenga wahusika ambao ndio wabebaji wakuu wa mawazo ya mwandishi. Nafasi ya lugha katika kuendeleza dhamira ya uozo katika riwaya tunayoishughulikia inaweza kuonekana katika pande mbili: lugha chafu na lugha safi (teule)

*Muundo na msuko:* katika riwaya hii itaonekana kwamba nguli Kemathi ndiye anayefungua hadithi. Mwandishi anaanza kwa kuyahadithia matatizo yanayotokana na uovu wa ufisadi na kisha hadithi inaanza kukua na kuwaingiza wahusika waovu kama Chabare na Flora. Hapa ndipo dhamira ya uozo inajitokeza wazi. Kando na Chabare na Flora, wahusika wengine waovu wanajitokeza na kuonekana kutenda uovu wa kila namna. Kemathi ambaye hashiriki katika uovu, anajitahidi kuwashawishi wenzake kujiepusha na uovu lakini hafanikiwi. Pamoja na maovu mengine, hadithi inakwisha baada ya kuonyesha uovu wa Chabare na Flora ukikomaa na kusababisha tanzia ya vifo vya wawili hao.

*Dhima:* Mwandishi anapoanza kuandika huwa ana maswala anayoyawasilisha kwa wasomaji. Maswala hayo hayawezi kuwafikia wasomaji au kuwa na athari alizonuia mwandishi pasipo kuwako na njia ya kuyawasilisha. Hivyo, mwandishi huwateua wahuska na kuwapa majukumu fulani. Mwandishi anaweza kumpa mhusika wasifu fulani wa kimaumbile, lugha ya kipekee, mazingara maalum, mtazamo na itikadi ambazo zinamtambulisha kama mhusika binafsi. Mwandishi ndiye hasa anayetawala matendo, mawazo, sifa na kauli zote za mhusika. Chabare na Flora wamejengwa na kujitokeza kuwa watenda maovu. Wamepewa vitendo hivyo viovu kwa makusudi na mwandishi ili kuunda dhamira lengwa.

*Maudhui:* Dhamira kama sehemu ya maudhui huweza pia kujitokeza katika maudhui. Dhamira ikiwa ndilo wazo kuu linalotenda au kujitokeza katika riwaya nzima, huashiriwa na mfululizo wa vijiwazo vinavyoweza kuoanishwa na kuunganishwa kutoa wazo moja. Vijiwazo hivyo hujitokeza katika kila sehemu inayoikamilisha riwaya.

*Uhamasishaji:* Dhana hii hutumika kueleza sababu zinazowafanya wahusika wayatende mambo fulani. Ni msukumo wa aina fulani. Mtu anayetawaliwa na msukumo wa tamaa kwa mfano, anakosa kuwajali wengine na hivyo kudhihirisha uovu wa namna hiyo.

Uovu pia hujitokeza katika *mitazamo* ya wahusika. Hapa tunachunguza: Je, wahusika waliopo wana mitazamo ya aina gani? Tunaangalia kwa mfano mielemeo yao ki-itikadi au kimaadili pamoja na saikolojia zao kama wahusika.

Wahusika kama viumbe wanaotumiwa na waandishi kuyatekeleza majukumu fulani na tofauti tofauti huwa na sifa zinazofungamana na majukumu yao. Kwa msingi huu, wahusika huainishwa au hugawika katika makundi mbali mbali kama vile: Mhuska bapa, mhusika bapa sugu, bapa kielelezo, mhusika batili, mhusika duara, mhusika ghibu, mhusika jumui, mhusika kipokeo, mhusika kani, mhusika mchomozi, mhusika mkuu, mhusika mdogo, mhusika msimulizi, mhusika shinda n.k. Kazi hii haitaingilia makundi haya ya wahusika. Tutajibana tu katika uhusika ulivyotumika kuendeleza uovu. Hivyo tutachunguza wahusika waovu na wahusika wema.

## 3.1.0 Wahusika Waovu Katika Riwaya ya *Upotevu*

Katika kazi yake, Mwenda Mbatiah ametumia wahusika wenye tabia na matendo maovu. Wahusika wanaoongoza katika kuendeleza dhamira ya uozo ni Chabare na Flora. Flora ni mwanafunzi katika chuo cha ualimu cha Mashariki, naye Chabare alifanya kazi katika afisi ya Kilimo. Matendo ya wahusika hawa ni maovu kuanzia mwanzo hadi mwisho. Chabare na Flora wanaweza kubadilishana majina kwa vile matendo na fikira zao ni sawa. Wote wawili ni wapenda raha za jiji na hawataki maisha ya mashambani. Flora anapofunga

shule, anafululiza moja kwa moja hadi jijini anakoishi Chabare. Anapoulizwa habari za kwao Murang'a na Kemathi, anajibu kwamba huko ni ushamba na ushenzi, na hivyo basi ni mahali pasipofaa kuishi.

Kwa upande mwingine, Chabare anakataa kuchukua likizo yake mwezi wa Disemba. Anafanya hivyo ili awe na wakati mzuri wa kukaa Nairobi wakati huo bila kusumbuliwa na shinikizo za kumtaka kwenda nyumbani. Wanapokutana, Chabare anamweleza Flora kuwa, "Nilitaka Disemba hii nikae Nairobi na mpenzi wangu – *to enjoy life*." (uk. 52). Aidha, mwandishi anatueleza kwamba hakuna njia nyingine ya kujistarehesha aliyoipenda Flora kama kucheza densi. Hili ndilo jambo mojawapo lililomvutia jijini Nairobi na kumfanya ayachukie maisha ya shamba.

Chabare naye alikuwa ni mpenda anasa, na hasa wanawake. Sura yake ilikuwa na mvuto mkubwa kwa wanawake, aliwawinda warembo mara nyingi lakini uchu wake haukutosheka. Tunaarifiwa kwamba Flora alikuwa na tabia hiyo hiyo. Akiwa shuleni alikuwa ameavya mara mbili. Anapoizungumzia tabia ya Flora, mhusika Pamela Kagendo, anasema kuwa: "Flora ameharibika kabisa kitabia tangu zamani ---- mbali na kuwa kigeugeu na mwenye dharau, Flora ana tabia za Malaya." "lakini huoni Chabare yuko hivyo hivyo!" Kemathi alimaka (uk. 77)

Flora, ingawa ana urafiki na Chabare, ana wanaume wengine wengi. Kwa kuwa siku za mwizi ni arobaini, siku moja, Flora akiwa anatoka katika uhusiano wa kimapenzi na afisa mmoja wa polisi, alifika nyumbani na kumfumania Chabare akizini na mhudumu wa nyumbani wa jirani yao. Keremi nduguye Chabare, alipokuwa akizungumzia tabia ya

wawili hawa, anazungumza kama mtu aliyekwisha kukata kauli kutosikitikia uozo wa kitabia wa Flora na Chabare (UK. 112). Hii ni imani thabithi kwamba uozo huo ulikuwa donda ndugu kwao. Inashangaza kuwa Flora alikasirika kwa kumfumania mpenzi wake akiyatenda yale ambayo yeye mwenyewe alikuwa akiyatenda.

Flora ni mwingi wa uozo kitabia, Chabare ambaye ni mpenzi wake, baada ya kuzoeana na yeye, anakiri kwamba Flora ni mkaidi na mwenye dharau. Ana moyo wa kigeugeu; dakika hii ni bashasha, dakika nyingine amenuna; mara ni mpole na mkunjufu; mara amefura kwa hasira n.k. Flora ni mwenye ulimi mchafu na usokuwa na nidhamu. Wakiwa katika starehe zao za tafrija huko Ndotomu, kulizuka vurumai. Chabare alipomwacha Flora na kwenda kudensi na Maria, rafiki yake Kemathi, Flora alilipuka na kuwasomea vikali wawili hao kama ilivyo hapa chini:

> "We mpumbavu unaniacha halafu unakuja kucheza na huyu Malaya?" Flora alihujumu "Ala! Hiki kitakataka kinaniita Malaya?" Maria alikuja juu kwa kelele."Malaya! Unataka kuninyanganya *boy friend* wangu?" Flora aliropoka. (uk 61).

Hili ni thibitisho kuwa Flora ana lugha chafu. Pia alimtukana Keremi , ndugu mdogo wa Chabare kuwa yeye ni kandamnasi. Ni mwanamke mfyosi na mwenye kigeugeu. Vile vile, Chabare anaonekana kuwa na ulimi mchafu, anawaita wazazi mafala kwa sababu ya misimamo yao ya kimaadili.

Aidha, Ngotho babake Flora, alipojaribu kudokeza kwamba alituhumu Chabare alihusika na kifo cha mtoto wake, Chabare analipuka na kumtusi. Alimwambia aache kuongea maneno ya kilevi na kipumbavu. Kulipozuka uzushi kuhusu ulipaji wa bili ya hospitali ya Flora; Chabare anamtukana Ngotho kwa kumuita 'kizee kisafihi' (uk. 105). Hapa basi ni kweli kuwa mwandishi anaendeleza dhamira ya uozo kupitia kwa lugha waitumiayo Chabare na Flora.

Imedhihirika kuwa wahusika wote wawili hawa hawateui lugha yao kiungwana kama inavyodai nadharia yetu. Nadharia ya Maadli inasisitiza kwamba wenye maadili ni wenye kujifunza lugha teule iliyotumika na kunukuu kauli takatifu kutoka vitabuni. Hivyo, hawa ni wahusika waovu ambao tabia zao hazifai kuigwa na wasomaji.

Chabare na Flora wana tabia ya udanganyifu. Flora alipokufa, Chabare hasemi moja kwa moja kilichomuua Flora. Keremi ndiye aliyemfichulia Kemathi chanzo na kiini cha kujiua kwa Flora. Tunamwona Flora pia akimdandanya babake kuwa anakwenda Mombasa kwa dadake ilhali anaenda jijini kwa Chabare.

Isitoshe, Chabare ana unafiki, unafiki ni hali ya kujifanya kuwa ni rafiki na hali ni adui; hali ya kutokuwa mkweli. Mwandishi anatueleza kuwa Flora alipokufa, Christine alikuja kuchukua nafasi yake usiku huo huo. Kemathi, katika kuliwazia jambo hili, alikisia kwamba labda Chabare alilala na Christine siku iliyofuatia kifo cha Flora. Alihisi kwamba angesubiri mpaka angalau aliyekufa azikwe, kisha mengine yafuate baadaye. Keremi wakiwa na Kemathi, anamweleza kwamba mapenzi baina ya Christine na Chabare ni ya kiendawazimu

kama ilivyokuwa Flora alipokuwa hai. Dalili za Chabare kubadilika kitabia hazionekani kabisa. Hili ni dhihirisho kwamba uozo wake ulikuwa umepita mipaka.

Wahusika Chabare na Flora wanaonyesha sifa zinazowiana na dhamira ya uozo inayoendelezwa na msimulizi wa kazi hii tunayoishughulikia. Wahusika hawa ni kama jira ambapo dhamira hiyo ya uozo inazungukia. Jambo hili linatupelekea kuamini kuwa wahusika hawa wanaoongoza katika kuendeleza uovu wameumbwa na kupewa majukumu ya kuendeleza uovu.

Mwenda Mbatiah anawatumia Chabare na Flora kupiga vita tabia fulani zisizokuwa na nafasi katika jamii yake. Mwandishi anadhamiria kuonyesha kwamba malezi anayoyapata au anayoyakosa mtu utotoni, yanachangia kitabia Katika utu uzima. Flora kwa mfano, hakupata malezi bora akiwa mtoto, jambo ambalo linachangia kudidimia kwake kitabia. Mtunzi pia anatuonyesha wahusika ambao hawahisi wala kujaribu kutatua shida za ulimwengu wanamoishi.

Kuna wahusika Getonga na Moronge ambao ni watoto wa kwanza wa Nabea, babake Kemathi. Matendo yao yanaashiria uozo wa namna tofauti tofauti. Getonga ambaye ni kifungua mimba, alikuwa afisa wa kilimo wilayani Meru. Alifuatwa na Moronge ambaye alikuwa karani katika ofisi ya Mkuu wa Wilaya mjini Meru. Wazazi wa watoto hawa waliwasomesha wakitumai kuwa wakimaliza masomo na kupata kazi wangeweza kuwasaidia na kuufuta ufukara wao. Sivyo iwavyo, wanapopata kazi wawili hao kinyume na baba yao, wanaishia kuwa wachoyo na wasiopenda kushirikiana.

Babake Getonga na Moronge alikuwa karimu na aliyependa kushirikiana na jamaa zake. Tulitarajia kwamba watoto wake waweze kuiga tabia zake, lakini tunaelezwa kwamba hata karo ya Mbaabu walikataa kusaidia kulipa. Kemathi aliyaona matatizo mengi katika familia yao kuwa na chanzo chake katika kaka zake kushindwa kusikilizana na kuwasaidia wazazi na ndugu zao. Walikuwa katika mashindano ya kutafuta utajiri.

Ndugu hao walizua pingamizi dhidi ya Kemathi kuendeleza masomo yake. Tunaelezwa kwamba:

> Tangu mwanzo, baadhi ya jamaa hao walipinga hatua ya kuendelea kwake na masomo baada ya kupata digrii ya kwanza. Hivyo basi mambo mengi aliyoyasema kuhusu masomo yake waliyaona kuwa ni ya kiwendawazimu. (uk.11)

Wanamwonea Kemathi wivu kwa sababu ya kisomo chake. Ni tabia kwa kweli ambayo haifai kwa sababu mmoja wa wanajamii anapopiga hatua na kustawi, hunufaisha jamii nzima katika huduma zake.

Wawili hawa wana tabia inayotajwa riwayani kuwa ni tabia ya 'wizi.' Kupitia kwa barua ya Mbaabu kwa Kemathi (uk. 130), tunagundua kuwa baada ya kifo cha baba yao, Getonga na Moronge wana njama ya kugawanya mali ya marehemu baba yao baina yao wawili tu. Hawataki kuwahusisha watoto wengine. Ni njama anayoieleza Mbaabu kuwa ni hatari. Ili

waweze kufaulu katika kutekeleza uovu huu, waliwagawia wazee wa kijiji pesa pamoja na chifu ndipo waweze kuwaunga mkono. Wana tabia ya kutoshirikiana kwa mambo mazuri ila wanapokuwa katika njama fulani.

Wamitila (2002:55), akilizungumzia suala la 'dhamira na uhamasishaji' anatueleza kuwa katika kutenda mambo, wahusika huwa na sababu zinazowafanya watende mambo fulani; yaani huwa na msukumo wa aina fulani. Hivyo basi, kulingana na tuliyoyasema hapo juu, kuna ithibati tosha kuwa matendo ya Getonga na Moronge yanachochewa na tamaa ya kupata mali na kutajirika.

Waaidha, wahusika hawa wawili wana chuki. Kemathi anaelezwa na mamake kwamba, "alipoipinga mipango miovu ya Getonga na Moronge, walimchukia sana, na tangu siku hiyo hawaongei tena." (uk. 140). Wahusika hawa wamekosa utu, wakati wa Krismasi hawamwaliki mama yao kusherehekea pamoja na familia zao. Mama yao yuko peke yake jikoni, tukio ambalo lilimstaajabisha Kemathi alipotoka jijini na kumpata mama katika upweke huo.

Wahusika wengine waliotumiwa na mwandishi kuendeleza uozo ni Ngotho na mtoto wake wa kiume Ndung'u. Mhusika Ngotho hajitokezi katika kurasa za mwanzo za riwaya, tunakutana naye baadaye, wakati ambapo Flora amefariki. Mzee Ngotho alikuwa babake Flora, na Ndung'u alikuwa ndugu mdogo wa Flora.

Mwandishi amewasawiri Ngotho na Ndung'u kisanaa hivi kwamba kwa kuwaona tu, taswira ya uovu inaanza kujengeka akilini mwa wasomaji. Tunaelezwa kwamba; "Kilichojitokeza zaidi katika uso wa Ngotho ni mkunjamano wake wa kudumu, uliompa mtu yeyote

aliyemtazama wazo kuwa mwenye uso huo alichukizwa na kila kitu alichokiona." (uk. 89). Naye Ndung'u alikuwa mrefu mwembamba kama uzi. Mara tu Kemathi alipomwona, jina la mbwa koko lilizuka akilini mwake. Wahusika hawa wawili wamepewa wasifu wa kimaumbile unaooana na majukumu waliyosawiriwa kuyatekeleza.

Kila wanapotajwa wahusika Ngotho na Ndung'u, vitendo vyao viovu vinadhihirika wazi wazi. Ngotho alituhumu kuwa Chabare alihusika katika kifo cha mtoto wake Flora bila kufanya uchunguzi wowote. Ngotho na Ndung'u walikwenda kuripoti kwa polisi kuwa walimshuku Chabare kwamba alihusika na kifo cha Flora. Baada ya kudadisiwa na polisi, Keremi anakiri kwamba Ngotho na mwanawe walitumia hila nyingi kuwashawishi polisi kuchukulia kuwa Chabare alihusika na kifo cha Flora. Jambo ambalo lilimpelekea Chabare kutiwa korokoroni. Tunaarifiwa kwamba Keremi, nduguye Chabare, aliwaona wawili hao kama mashetani ambao walifurahia kuwaingiza mashakani wasiokuwa na hatia. (uk. 104)

Kama waovu wengine, tabia ya ulevi iliwasibu. Walipokuwa katika mchango wa kutafuta pesa za kulipa bili ya Flora ya hospitali, Ngotho anapopewa wakati wa kuzungumza, matamshi yake yalisindikizwa na harufu kali ya pombe. Ameathiriwa pia na dhana potovu kuwa waliostaarabika ni wenye kutumia Kiingereza. Katika mazungumzo yake, aliwastaajabisha wale waliomsikiliza kwa kutumia Kiingereza (kibovu) ambacho hakukimudu ipasavyo. Alikosa utu hivi kwamba hakujali maslahi ya akina mama ambao hawakuelewa Kiingereza. Shughuli ya kuchanga pesa ilipoendelea, alitarajiwa atoe mchango mkubwa zaidi kuliko wengine kwa sababu msiba ulimhusu. Ajabu ni kwamba aliwashangaza na kuwaaibisha watu waliokuwepo kwa kutoa noti ya shilingi mia mbili. Hataki kushirikiana na wengine katika kutatua mzozo wa tanzia ya Flora.

Ngotho pia ni mchokozi na mwenye dharau. Wakiwa kwenye mkutano, Christine aliomba kwa heshima na unyenyekevu aruhusiwe kwenda kazini usiku huo. Ngotho hakuwa na subira alimrushia maneno:

> "Unaenda kazi usiku?" Ngotho aliuliza kwa dharau.
> "Ndiyo, wakati mwingine - kama leo - zamu yangu inakuja usiku," Christine alijibu kwa upole. "Kazi gani hiyo? Kwani wewe ni mlinzi? Sijawahi kusikia kwamba wanawake wanafanya kazi ya ulinzi!" (uk. 92).

Ngotho alimuudhi sana Christine ambaye alikuwa ni mhudumu katika hoteli maarufu ya watalii – *Kencity*. Kemathi anamwambia ayapuuze matusi ya kizee kiendawazimu.

Isitoshe, kulizuka ubishi kuhusu aliyefaa kulipa bili ya hospitali ya marehemu Flora. Chabare alieleza kuwa alikuwa ametimiza wajibu wake kwa kulipa elfu hamsini na kuwataka Ngotho na jamaa zake kulipa fedha zilizosalia. Ngotho kwa kusikia hayo; aliangua kicheko kwa sauti ya juu. Kilikuwa kicheko cha kishetani ambacho kilimshangaza kila mtu. Alikuja juu kuwa hawangeweza kulipa pesa hizo kwa sababu hawakuhusika na kifo cha Flora. Wote waliokuwa kwenye mkutano walikubaliana kwamba Ngotho alikuwa mzee mjinga na mwovu. Baadaye, Ngotho anamtisha Chabare kuwa: "Usipozilipa pesa hizo, *you'll see fire*" (uk. 105)

Chabare naye anakana kuwa hatalipa pesa hizo kisha Ndung'u anaingilia kati kwa kusema: "Mtu ambaye atalipa pesa hizi si mwingine bali ni wewe Chabare upende usipende!" (uk.105)

Kutokana na kisa hicho, mwandishi anadhamiria kutuonyesha jinsi ambavyo wahusika hawa walikosa staha kwa marehemu Flora. Hawakumheshimu Flora tena. Walichokithamini sasa ni pesa. Aidha, Kemathi anakiri kuwa watu hawa ni waovu na kuona tukio hili kama kilele cha upotofu wa kizazi chake.

Wakoloni wanadhihirishwa na mwandishi kuwa na mfumo wa kimabavu na kiubaguzi wa rangi. Mfumo huo unaonekana kutokwisha hata baada ya ukoloni. Ni mfumo waliourithisha kwa askari wa serikali za baada ukoloni. Serikali za kikoloni ziliwatumia polisi kuwapiga Waafrika na kuwadhalilisha ili wawatii wazungu na kuwaogopa. Baada ya uhuru, askari wana tabia sizo hizo. Polisi hawana heshima kwa raia na zaidi ya hayo, wanawafanyia dhuluma nyingi.

Aidha mtunzi anawasawiri askari kama vikaragosi, wafidhuli na watu waliofurahia kutesa watu na kuitisha hongo. Kila wanapoabiri gari, nauli hawalipi. Wakiingia baa wananunuliwa pombe. Kuna abiria mmoja (uk. 8) anayelalamikia na kuikashifu vikali tabia hiyo huku akiita tabia ya kimalaya. Anashikilia kwamba wanaopewa vitu vya bure ni malaya. Kemathi anayaona haya yote kama maovu ya maisha ambayo hayana kikomo.

Uovu unaendelezwa pia na matajiri. Tajiri mwenye jengo la Gethongori anakoishi Kemathi, ni mmoja kati ya wachache wasiojua uchungu wa maradhi ya umaskini. Matajiri hao wanaelezwa kuwa hawana utu. Mwandishi anasimulia kuwa utajiri na utu vilikuwa kama mafuta na maji, havipatani. Mazingira ya majengo hayo yaliyowapa hela nyingi matajiri walioyamiliki, yalijaa uvundo wa takataka zilizoozeana . Kutosafisha mazingira ambamo wateja wa biashara yao waliishi ni ukosefu wa utu.

Chifu M'Ngaroni ni mhusika mwingine ambaye anaendeleza dhamira ya uozo. Kiongozi huyu alikuwa mtu mkaidi aliyependa kuhongwa na hivyo kutotoa huduma ya haki kwa wananchi. Mbaabu anapomwandikia Kemathi barua, anamweleza kuwa ndugu zao, yaani Getonga na Moronge wamewagawia pesa wazee wa kijiji pamoja na chifu ili wawaunge mkono katika njama zao. Mbaabu anahofia kwamba hata akimwendea Bwana Chifu kumkomesha uozo huo, hatamsikiliza kwa sababu ya ujana wake na zaidi kwa sababu amehongwa. Kweli katika jamii iliyooza kama hii ya akina Kemathi, wanakijiji wengi walihusudu pesa huku wakiongozwa na viongozi wao katika uozo huo.

Kemathi alipoarifiwa na Mbaabu kuhusu hila za chifu, yeye, Mbaabu, Kagweria na mama yao walipanga kwenda kumwona chifu. Mwandishi anasimulia kwamba:

> M'Ngaroni aliwakaribisha wageni waliomtembelea asubuhi ofisini mwake. Moja kwa moja, Kemathi alianza kusema kwa niaba ya wenzake, akaeleza haja yao kwa kifupi. Chifu aliona haya, akainamisha kichwa chake kilichojaa mvi Kemathi alipomfichulia wazi wazi kwamba alifahamu kuwa Getonga na Moronge walikuwa wamemhonga . Mama aliyathibitisha maneno ya mwanawe. (uk.144).

Tulitarajia chifu M'Ngaroni kuleta maelewano baina ya pande mbili zinazosozana yaani Kemathi na wadogo wake na ndugu wawili wakubwa. Kile Mbatiah anachosisitiza kupitia

kwa chifu ni kuwa mtu anayestahili kuongoza watu ni yule aliye na uwezo mkubwa wa kutatua matatizo ya watu anaowaongoza.

M'Ngaroni hatendi haki, yeye ni mfano wa viongozi wanaoonekana kuthamini fedha kuliko kitu kingine chochote. Anavunja sheria kwa kufanya mapendeleo katika huduma zake kwa umma. Yeye kama mtumishi wa serikali, anafaa kuwa kielelezo bora cha maadili cha kuweza kuigwa, hapaswi kuunga mkono ukiukaji wa sheria za nchi. Haya ni baadhi ya matukio yanayothibitisha uhaba wa uadilifu na kuchanua kwa ua la upotevu. Tunaambiwa kwamba visima vya maadili vilishakauka, nchi ikawa jangwa lililotapakaa ubinafsi na uroho (uk. 144). Tunakubaliana na mwandishi kuwa maadili hayamei katika jangwa bali huhitaji rutuba ya uongozi bora. Uongozi ambao hauonekani kuwepo katika jamii hii.

Mwanamke jirani ya Kemathi pamoja na mume wake ni wahusika wengine wanaodhihirisha tabia zisizofaa kuigwa. Mwanamke huyu anavaa kwa namna ambayo inashangaza. Mitindo yake ya mavazi ni sahili inayomwacha nusu uchi. Anatokeza akiwa amejifunga leso ndogo kiunoni huku sehemu yote ya juu ya mwili wake ikiwa wazi. Kemathi anamweleza Mbaabu kuwa mwanamke huyo ana tabia za kimalaya. Mbaabu anakiri kwamba alikuwa amesikia hadithi nyingi sana kuhusu wanawake wa Nairobi lakini alikuwa hajapata ithibati ya ukweli wa hadithi hizo. Sasa aliweza kujionea mwenyewe.

Mwanamke huyo alikuwa na watoto watatu na alitarajiwa kutoa mfano bora wa kimaadili kwa binti zake lakini inatukia kinyume. Mumewe pia ni mnywa pombe, hatulii nyumbani. Anaingia nyumbani usiku wa manane kutoka vilabu vya pombe na hatoi malezi bora kwa familia yake. Hivyo anachangia pakubwa katika upotofu wa maadili katika kiwango cha

familia. Kupitia kwa hii familia, mwandishi alikusudia kutuelimisha kuhusu umuhimu wa malezi bora katika familia. Familia ndizo zinazojumuishwa na kuunda jamii. Uozo unapoanza katika familia, jamii inayoundwa na familia hizo ni potevu.

Mhusika mwingine ni Maria ambaye ni kachero mwenye cheo cha Inspekta Mkuu. Ni askari kanzu anayeogopwa kuchumbiwa na wengi kwa sababu ya kazi aifanyayo, japo ana sura nzuri. Maria ana watoto wawili, kuliko tafrija hakosi na ni mnywaji wa vileo. Anacheza densi na Kemathi na mavazi yake hayasitili sehemu zake zote za mwili. Kanzu aliyoivaa ilikuwa na mkato wa V ambao ulionyesha sehemu ya juu ya mwanya baina ya maziwa yake makubwa. Aidha nguo hiyo ilikuwa fupi kiasi kwamba alipoketi kunywa bia, ilijivuta kwa juu na kuyaacha nje mapaja yake manene (uk. 58). Hii ni mitindo ya mavazi waliyoiga Waafrika kutoka nchi za magharibi bila kuielewa vizuri.

Vile vile, Maria anaendeleza uovu kwa matumizi yake ya lugha chafu. Wakiwa kwenye tafrija ya Ndototamu, Flora alimtusi kuwa yeye ni Malaya, Maria anasema:"Ala! Hiki kitakataka kinaniita Malaya?" Maria alikuja juu kwa kelele. (uk.61). Hapa, kwa kuangalia lugha anayoitumia mhusika huyu, tunaona kwamba lengo la mwandishi la kutuelekeza kwenye dhamira ya uozo linajitokeza. Kimani na Chimerah (1999:130), wakizungumzia nadharia ya Maadili wanasema kuwa, kuna lugha safi na lugha chafu. Wenye maadili wateue na kutumia lugha safi.

Riwaya ya *Upotevu* ina wahusika wengine wadogo ambao ni waovu. Kama vile Kegonda, Keremi, Mbaabu na Muthomi. Kulingana na Mong'eri (2000:45), Riwaya ya *Kusadikika* ina mhusika Majivuno aliye waziri mkuu. Majivuno lina maana ya kiburi au maringo.

Majivuno amechorwa kama mtu anayejisifu kwa madaraka aliyo nayo. Mhusika Kegonda katika riwaya ya *Upotevu* ana tabia sawa na mhusika Majivuno. Kegonda alikuwa kijana mwenye maringo ambaye alikuwa amenunua gari na kujivunia gari hilo. Tunaelezwa kwamba alipenda kupita vijijini na kulionyesha gari hilo. Mbaabu naye alipenda mambo ya wasichana na vileo alikunywa. Keremi nduguye Chabare ni mmoja wa wale wanaoshinda kwenye baa wakiwa na rafiki yake Koome hadi saa tatu usiku.

## 3.2.0 Wahusika Wema Katika Riwaya ya *Upotevu*

Nguli katika riwaya ya *Upotevu* ni Kemathi. Kemathi alikuwa kijana wa miaka ishirini na mitano aliyekuwa katika mwaka wa pili, akisomea digrii ya pili - uzamili. Kupitia kwa mhusika huyu, Mwenda Mbatiah, anawasilisha uadilifu katika maisha ya binadamu. Kemathi, ingawa yumo katikati ya wahusika wengi wanaotenda vitendo viovu, anachukua mkondo tofauti. Mwandishi anamsawiri Kemathi kama mtu ambaye hakuwa msemaji ila tu panapokuwa na suala nyeti. Alipenda sana mambo ya vitabu na mijadala kuhusu masuala ya kitaalamu. Kwake chumbani, mlikuwa na riwaya kama hamsini za Kiswahili na za Kiingereza. Alikuwa amezisoma zote na alikuwa hodari katika kujibu maswali ya fasihi. Kemathi alitumia wakati wake vizuri na kila alipochekwa na hirimu yake kwa "kutojua raha za pombe," aliwajibu kuwa bei ya bia tatu ingeweza kununua riwaya.

Kemathi ana utu na maadili. Alipata malezi mema na hivyo kujifunza mambo mengi mazuri kutokana na wazazi wake. Kutia bidii kazini ilikuwa mojawapo ya maadili mengi aliyojifunza kutokana na babake Nabea. Mbaabu alimwandikia barua ya kumweleza hisia za mama yake za kutaka aende nyumbani wakati wa Krismasi. Kwa kuwa Kemathi hakutaka

kumuudhi mama, anatafuta mbinu za kumfanya aelewe kwamba kazi nyingi za masomo ndizo zilizomzuia kufika nyumbani. Katika masomo yake, Kemathi ni mwanafunzi bora mwenye azma ya kuwa mhadhiri na mwandishi. Dhamira yake ilikuwa kutaalamika katika somo la Kiswahili na alikuwa ameanza kuandika mswada wa riwaya. Alitaka kutumia mswada huo kujieleza alivyohisi na alivyoona.

Kutokana na utu wake, Kemathi aliona wazalendo wakipigwa kikumbo na kunyamazishwa ili sauti zao zisiufungue umma macho. Aidha, aliona vijana wengi wasiokuwa na wazazi wakiangamizwa na dawa za kulevya na pombe. Haya ndiyo baadhi ya mambo yaliyomkera na hivyo kutaka kuyakemea kupitia kwa mswada wa riwaya yake. Kutokana na busara yake, tunamwona Kemathi akimshauri Mbaabu kuhusiana na masomo yake. Anamweleza kwamba:

> Naonelea kwamba ukishakata shauri kuhusu taaluma unayoitaka, kitakachobaki ni wewe kutia bidii katika masomo yanayohusiana na taaluma hiyo. Kama unataka kuwa mhandisi, lazima uwe mweledi wa fizikia na hisabati. (uk.17)

Vile vile, Kemathi ana nia ya kumsaidia mtoto wa Maria kupita mtihani kwa kumfunza. Anamfundisha Ben Kiswahili na kumpa mazoezi huku wakikutana mara tatu kwa wiki. Maria anapomuuliza malipo atakayohitaji, anasema hamlipishi, alitaka kumsaidia tu kama rafiki. Huu ni ushahidi tosha kuwa Kemathi ana roho safi ya kuwatakia wengine ufanisi na hakuwa na tamaa na uroho wa pesa.

Kinyume na wengine, mwandishi anatuarifu kwamba Kemathi hakutumia pesa zake vibaya. Ingawa alikuwa hajapata kazi rasmi na aliyategemea marupurupu waliopewa chuoni, desturi yake ya kukabiliana na tatizo la kutokuwa na pesa za kutosha ilikuwa ni kuyapanga mambo kwa uangalifu mkubwa. Aliziingiza pesa kidogo alizopata kwa yale mambo tu aliyozipangia (uk. 40). Aidha, Kemathi alishirikiana ipasavyo na wazazi wake. Licha ya kupata pesa kidogo kila mwisho wa mwezi, alichangia katika kulipa karo ya Mbaabu. Wakati mwingine, alimtumia mama pesa za matumizi nyumbani na wakati mwingine kumtembelea na kumjulia hali kwao nyumbani. Kupitia kwa matendo ya mhusika huyu, mwandishi anatuchorea taswira ya binadamu mwenye utu anayefaa kuigwa .

Kando na hayo , Oki- Ojok baada ya kuisoma hadithi ya Kemathi, aling'amua kwamba kijana huyo alikuwa na akili fahamivu, na maoni yake yalikuwa mazito. Alimwona kama kijana aliyeelekea kutetea haki ya wanyonge katika jamii. Kemathi ana misimamo thabiti, ana marafiki wengi wanaokunywa pombe kama vile Muthomi na Chabare. Wakati mwingine aliketi nao wakilewa na hata wakati mwingine aliwanunulia bia lakini yeye alikunywa soda au kahawa. Mwandishi anatuarifu kuwa kilichomvuta kwao zaidi ni mazungumzo na kushiriki katika mijadala. Siku moja, wakiwa katika hoteli, rafiki yake Muthomi alimuuliza kuhusu urafiki wake na Maria na kama atamwacha Pamela Kagendo. Kemathi alimjibu, "Mimi sio mtu wa kuyumbishwa na wanawake. Nampenda Kagendo wangu na tutaoana hivi karibuni." (uk. 71)

Dondoo hili ni ithibati kwamba binadamu ana uwezo wa kipekee wa kutawala hisia zake inavyodai nadharia yetu ya Maadili. Hivyo, nasi tunaafikiana na mawazo haya kuwa mtu ana uwezo wa kuwajibika akitaka. Kemathi, licha ya kuwa katika mazingira ya hali ya

maisha ya uovu, na ambayo yangemvuta kwa urahisi, aliweza kusimama imara na kuwa kielelezo chema cha maadili.

Hali kadhalika, Kemathi ana mawazo tofauti na wanaume wengi kuhusu itikadi. Wakiwa basini kuelekea jijini, Kemathi anamwambia mkewe kuwa : "Hata sisi wanaume wa kizazi hiki hatutaki wanawake kudhulumiwa. Maisha ya leo yalivyo, lazima mke na mume kushirikiana ." (uk.76) Mwanamke aliyeketi kando ya wawili hawa na aliyeyasikia mazungumzo haya alisema:

> Kwa bahati mbaya sio wanaume wengi walio na msimamo kama wako kaka. Magamba ya mila na desturi bado yamewafunika macho. Elimu ya kisasa haijawafikia kuwafungua macho. (uk.77)

Mazungumzo haya yanaonyesha kuwa watu wa jamii hii walishikilia ukale; jambo linalomsukuma mtunzi wa riwaya ya *Upotevu* kuwafahamisha kuwa walihitajika kubadilisha hali yao ya maisha na itikadi zilizopitwa na wakati. Mchumba wake Kagendo akiwa mja mzito, Kemathi aliweza kuingia jikoni na kupika. Hili ni jambo ambalo lilimfanya Kagendo kumwona Kemathi kuwa mwanamume mwenye mawazo huru juu ya mgawo wa kazi baina ya mume na mke. Bado wanaume wengi walitawaliwa na itikadi potovu kwamba kazi za jikoni ni za mwanamke.

Isitoshe, Kemathi ana uvumilivu na uaminifu. Mara nyingi, Chabare alimuudhi kwa tabia zake mbovu lakini alimsamehe na kutovunja urafiki naye. Ni rafiki wa kweli ambaye hamtoroki Chabare wakati wa kifo cha Flora. Anafaulu pia kumshawishi Christine asiondoke na kumwacha Chabare pekee wakati ana msiba. Wanabaki wote wawili kumfariji Chabare. Aidha, Kemathi ana huruma kwa Chabare na anakiri jambo hili kwa kumwambia Keremi kuwa: "Namhurumia sana Chabare kwa mashaka yote haya. Natamani kuyaona yamepita." (uk.110). Hivyo basi, Chabare walipohitajika kufika katika kituo cha polisi cha Kasoko na nduguye Keremi, Kemathi anaandamana nao kwa sababu ya upendo na huruma. Rafiki ni anayekufaa hata na wakati wa dhiki.

Pia Kemathi alimhurumia Maria kwa matatizo ya maisha yake, hasa upweke. Maria anakiri wazi kwamba Kemathi alileta matumaini katika mustakabali wa mtoto wake Ben (uk. 130). Kila walipokutana, Maria alifurahi na kujawa na matumaini kwa kupata mtu wa kufungulia moyo wake uliojaa siri chungu za maisha yake. Kemathi hakuweza kumnyima furaha hii. Tunaweza kulinganisha tukio hili na kisa cha Utubora katika riwaya ya *Utubora Mkulima.* Utubora anasaidia kubadilisha hali ya Bimkubwa aliye na simanzi kwa kuwapoteza watu wote wa jamaa yake na sasa anaishi maisha ya upweke. Kupitia kwa juhudi za Utubora, hali ya Bimkubwa inabadilika kuwa nzuri

Kemathi anadumisha urafiki na mpenzi wake Pamela Kagendo. Anapopata mimba akiwa chuoni, wote wawili wanakubaliana kuwajibikia mimba hiyo. Kwa muda wa miaka miwili ambayo mapenzi yao yalikuwa yamedumu, Kagendo alikuwa na ithibati tosha kuwa Kemathi hakuwa na tabia ya udanganyifu (uk. 121). Mwandishi anamchora Kemathi kama mtu aliye na ujasiri wa kushikilia msimamo wake kuhusu suala lolote zito katika jamii. Alijiepusha na

mkondo wa mikabala pendwa. Kila mara, msimamo wake ulikuwa na misingi ya haki na utu.

Kemathi amedhihirisha ukamilifu wa mja. Ameonyesha sifa za kiutu kama vile kuwa na roho safi, kuwa na heshima kwa wenziwe, kuwa na akili nzuri na pia kuonyesha kuwajibika. Ingawa Kemathi ni mtu mwadilifu, mara nyingine anakabiliwa na majaribu. Majaribu hayo hayawi ya kudumu kwani baadaye yanashindwa. Kushindwa kwa majaribu hayo ni taashira ya nguvu za maadili dhidi ya maovu.

Oki-Ojok ni mhusika mwingine aliye mwadilifu. Oki-Ojok alikuwa mhadhiri hodari mwenye akili pevu ya kiusomi na kizalendo. Alisifiwa na wale waliobahatika kufunzwa naye kuwa ni mtu jasiri, na aliyewajibika kuliko wahadhiri wengine. Alikuwa na msimamo na itikadi thabiti isiyoyumbishwa. Tunaambiwa kuwa alikataa kununuliwa na wanasiasa ndipo wakamchukia na kutaka kumwangamiza. Biblia inatwambia kuwa hitaji kubwa la ulimwengu ni uwepo wa watu ambao watasimamia ukweli na kuiita dhambi kwa jina lake na kukataa kununuliwa hata mbingu iwaangukie. Watu sampuli ya Oki-Ojok ni wachache mno katika ulimwengu wa sasa.

Oki-Ojok alikuwa pia mwandishi na mwaguzi wa jamii yake. Aliwajibika kuzifasiri ndoto za kitaifa kwa manufaa ya umma. Kupitia kwa uandishi wake, alikemea uroho na ufisadi. Jambo hili lilimfanya afungwe kwa kuitwa mchochezi na msaliti, na hata alipotoka kizuizini, alinyimwa kazi. Alikuwa mzalendo halisi aliyeongoza juhudi za ukombozi wa jamii yake.

Pamela kagendo, mchumba wake Kemathi, ni mhusika mwenye adabu, karimu na mpole. Hali hii inamfanya kuwa tofauti na wahusika wengine. Urafiki wake na Flora ulikuwa urafiki

baina ya watu wawili ambao hawakulingana kitabia hata kidogo. Aidha, ni mwenye subira, Kemathi anapolala nje kwa Chabare, anangoja kuambiwa yaliyotukia bila fujo. Kemathi pia anakiri kwamba alimpenda Kagendo kwa moyo wake wote kwa sababu ya uaminifu na utu wake. (uk.134).

Mzee Nabea ni mnyenyekevu na mpenda haki. Walishirikiana na mkewe kuwasomesha watoto wao. Wawili hawa wana bidii katika kilimo. Wana msimamo thabiti kama wazazi. Nabea alichekwa na wazee wa rika lake kwa kutoshiriki katika anasa za dunia lakini aliyapuuza hayo na kujitegemea kimawazo. Alikuwa vile vile mshauri wa watoto wake, kwa mfano, anamwambia Mbaabu kwamba: "ukiyachezea masomo sasa, maisha yatakuchezea baadaye." (uk.16). Kemathi anakiri pia kwamba baba yao aliwakariria kila mara kuwa, "elimu ndiyo mambo yote." (uk.31).

Nabea ni mkarimu kiasi cha kuwakusanya jamaa na marafiki wakati wa Krismasi na kuwafanyia karamu kubwa. Kutokana na uadilifu wake, alipendwa na wengi, jambo ambalo lilithibitishwa na ukubwa wa umati uliokuja kutoa heshima za mwisho wakati wa mazishi yake. Mwandishi anasema:

> Ilikuwa kawaida kuwasifu watu wakati wa kuwazika, lakini waliohudhuria mazishi haya walihisi kuwa sifa nzuri za Nabea zilizoelezwa hazikutia chumvi wema wake. Kusema waridi ni ua zuri sio kipiga chuku bali ni kueleza ukweli. (uk. 38)

Kupitia kwa Nabea na mkewe, mwandishi anadhamiria kutuonyesha umuhimu wa uwajibikaji kwa upande wa wazazi. Wazazi hawa waliwalea wanao kwa upendo na walijitolea kuwaelimisha. Malezi aliyoyapata Kemathi, yalikuwa ni msingi muhimu wa uadilifu wake.

Ramachandra ni mhusika mwingine mwenye utu, ana huruma na roho ya kusaidia. Aliwapa Chabare na wenzake maelezo ya kuridhisha kuhusu taratibu za kufuata katika kutoa marehemu Flora na kwenda kumzika. Kwa kuwaonea huruma, yuko tayari kuwapa maiti na kuwakubalia wahusika kulipa bili baadaye. Kemathi ambaye  Kwa kawaida aliwaona Wahindi kama kupe waliopendelea kuwanyonya Waafrika baada ya uhuru, alimwona Ramachandra japo mhindi, kuwa mtu aliyejawa na utu.

## 3.3.0. HITIMISHO

Kwa jumla katika sura hii tumejadili namna uhusika ulivyotumiwa kuwasilishia uozo katika riwaya ya *Upotevu*. Tumechunguza wahusika waovu na wahusika wema. Idadi ya wahusika wema inaelekea kumezwa na ile ya wahusika waovu. Inadhihirika bayana kwamba uozo umezamili (umekita mizizi) kutokana na jinsi uovu umekiuka wema katika jamii ya riwaya ya *Upotevu,* kwani vitendo viovu vimejitokeza kuwa na nguvu kwa kushinda vile vya wema.

Uchunguzi huu umebainisha pia kwamba uhusika uovu huanza kwa hatua na kukua na kukiuka mipaka kadri wahusika wanavyozidi kutangamana na jamii. Pia, wahusika wamejengwa katika hali ya uhalisi huku wengi wao wakichangia sana kukuza dhamira kuu. Chabare na Flora ndio wahusika wakuu katika kulikuza suala la uozo na kulitoa kwa uwazi katika kazi hii. Hata hivyo, wahusika wote wamekuwa na michango tofauti katika kujenga

dhamira au katika kufikisha ujumbe wa mwandishi. Imebainika vile vile kuwa uovu mwingi uliojitokeza katika wahusika ulidhihirika katika vitendo, lugha, dhima, na uhamasishaji.

Aidha, kuna ukweli usiopingika kuwa uozo unaodhihirishwa na baadhi ya wahusika una chanzo chake katika malezi walioyapata na elimu waliyoipata. Tofauti kati ya wasomi na wale ambao hawajasoma haijitokezi. Inashangaza kuona kwamba wahusika waliosoma na hasa waliopata elimu ya chuo kikuu kama Chabare, Muthomi na Kegonda ndio wanaoongoza katika kueneza uovu katika jamii. Matarajio ya jamii kwa wasomi hao kuipa mwelekeo kutokana na kisomo chao yanaibuka kuwa ndoto/hayatimizwi. Elimu waipatayo vijana haiwasaidii kuboresha maisha yao, bali husaidia katika kuwaangamiza zaidi.

Uwepo wa maadili katika jamii hii ni jambo gumu kwani uozo umekolea na la kustaajabisha mno ni kwamba dalili za mabadiliko hazionekani. Wahusika waovu hawashiriki katika utatuzi wa matatizo yanayowakabili. Tunahitimisha sura hii kwa kusisitiza kuwa dunia ingekuwa mahali pazuri pa kuishi kama wanadamu wote wangethamini na kukuza sifa za kiutu kama huruma na moyo wa kusaidiana, badala ya kutumia kabila, rangi au hisia zao kama vyombo vya kujinufaisha wao na kuwagandamiza wengine.

# SURA YA NNE

## ATHARI ZA UOVU KATIKA JAMII

### 4.0.0 UTANGULIZI

Kimani na Chimerah (1999:26) wanasema; "kuyamulika matendo ya kimaadili kama "Mchumia juani hulia kivulini," "Mui huwa mwema" na kadhalika, hutuelekeza katika upande mmoja tu wa dhamira ya kazi ya fasihi." Waandishi hawa wanatuhimiza kuvuka mipaka ya kuangalia upande mmoja wa sarafu katika tahakiki zetu. Wanazidi kusema kwamba; dhima la mwandishi wa kifasihi ni kuwasilisha ukweli na uhalisi wa yale anayokumbana nayo. Msanii hutegemea hali halisi ipatikanayo katika jamii aizungumziayo.

Kazi ya fasihi si ya kuyaeleza yale yalio mema na yapendezayo kusikiwa bali ina jukumu la kuyaonyesha hadharani hata matendo maovu yajulikane, ili yapate kutafutiwa suluhisho. Mwandishi haishi kwa kuyamulika yale yaliyoko mbele ya pazia tu bali hulifungua pazia hilo na kuionyesha jamii hata yale yatendekayo nyuma ya pazia ili kuwazindua wanaopitia katika madhila mbalimbali waweze kujikomboa.

Hivyo basi, ni muhimu kuchunguza athari za uovu katika jamii ya riwaya ya *Upotevu.* Uovu ni kama pweza mwenye mikia chungu nzima. Kila mkia unaleta athari kubwa katika maisha ya binadamu. Kila mojawapo unatoa sumu ambayo inaangamiza mwenye kuutenda uovu huo. Hata ukiukata mkia mmoja, hutakuwa umefanya jambo kubwa, kwa sababu atabakia na mikia mingine na ataendelea kuleta maangamizo. Suluhisho la kimsingi ni kumteketeza

pweza mwenyewe. Utafiti huu unafanywa kwa misingi ya nadharia ya Maandili inayosisitiza kuwa athari ya hali ya maisha ya uovu ina mvuto mkubwa sana kwa watu wengi. Kwa hivyo, binadamu asipokuwa mwangalifu na mwenye misimamo thabiti dhidi ya uovu, anaweza kuyumbishwa holela na nguvu za uovu wenyewe.

Sura hii imejikita katika kuchunguza na kuonyesha madhara ya uovu katika jamii. Athari zitakazochanganuliwa ni zile ambazo zimejitokeza katika riwaya tunayoishughulikia. Athari hizo ni pamoja na: utabaka na umaskini, vifo, hofu ya kimaisha, athari za ukoloni, kutowajibika, magonjwa, vita, na kukata tamaa.

### 4.1.0 Utabaka na Umaskini

Utabaka ni kundi la watu linaloundwa na watu wenye sifa sawa za kiuchumi. Utabaka unaletwa na ile hali ya wachache kujilundikia mali ya kitaifa ambayo ingetumiwa kwa faida ya raia wote. Nao umaskini ni hali ya kukosa mali, ni ufukara au uhitaji.

Kenyatta ( 1978:314) anasema kuwa, maadili katika jamii hutegemea mfumo wa uchumi na wa kijamii. Kuvunjika kwa maadili kunaweza kuwa zao la mabadiliko ya kiuchumi katika jamii. Jamii ya riwaya ya *Upotevu* inadhihirisha mfumo wa utabaka. Mwanafalsafa wa Kijerumani Karl Marx alisema kuwa historia ya maisha ya binadamu ni ya harakati za kitabaka. Marx, akizungumzia maadili, alisema kuwa usawa miongoni mwa watu na kutenda haki kwa kila mtu ni mambo ambayo yanafaa kuzingatiwa na kila jamii. Kwamba kila mtu katika jamii pana ya watu ana haki kuheshimiwa na wengine au na kila mtu.

Unyonyaji, unyanyasaji, kutotendewa haki na uwepo wa tabaka linalomiliki mali na kutawala matabaka mengine ni mambo yasiyokubalika na nadharia ya Maadili. Nadharia hii

inasisitiza kuwa maadili yanafaa kudhibiti nyanja zote za maisha ya binadamu k.v kazi za kila siku, siasa, elimu, familia n.k. Hivyo maadili yadumizwe na watu wote na kama kutatokea mabadiliko yoyote katika jamii, yaongozwe na maadili. Ingawa Nyerere hakufaulu sana katika jaribio lake la kujenga ujamaa nchini Tanzania, angalau alikuwa ametambua kwamba utabaka ni ugonjwa. Mfumo wa kiujamaa ni ule ambao nyenzo za uzalishaji mali humilikiwa na wote. Jamii nzima hunufaika na ule usawa, mgawanyo wa haki wa mapato, na uchumi ni wa sawa.

Athari za ubepari ambao huthamini pesa sana huwafanya wasio na pesa kutaabika. Ubepari husababisha matabaka kwa kuwa ni wachache tu wanaomiliki rasilmali. Kuwepo na kuendelea kuwepo tabaka la juu hutegemea pakubwa tabaka la chini.

Katika mtaa wa Dandora anamoishi Kemathi, kuna jengo kubwa na maarufu la Gethongori. Tunaambiwa kwamba mwenye jengo hili alikuwa katika tabaka ambalo halikujua maana ya uhitaji wa pesa. Kila mwezi alipokea pesa nyingi kutoka kwa wateja wake waliopangisha nyumba zote kumi na mbili. Utabaka unadhihirishwa pia na maelezo ya mwandishi yafuatayo kuhusu hospitali ya Ramesh:

> Hospitali ya Ramesh ilikuwa mojawapo ya
> hospitali kubwa zaidi, maarufu zaidi na ya
> kisasa zaidi katika jiji la Nairobi. Ilikuwa
> katika mtaa wa Parklands, walikoishi Wahindi
> wengi na waafrika wa tabaka la juu. (uk 101)

Ni dondoo linalotuthibitishia kwamba ukweli jamii hii ilikuwa imegawika kuwili na hivyo kwenda kinyume na inavyodai nadharia ya Maadili. Utabaka huu una chanzo chake katika ubinafsi, ufisadi na ile hali ya wachache kujilundikia mali pamoja na kuzorotesha uchumi.

Katika jamii hii ya Kemathi, maradhi ya ufukara yalikuwa yamewasakama wengi hasa vijana. Mwandishi anaeleza kuwa, maradhi ya ufukara yaliendelea kufyonza uhai wa nchi. Maradhi yalitokana na ufisadi na sera ambazo hazikuwa na kichwa wala miguu (uk. 5). Kemathi, ni mmoja wa wale waliojikuta katika mtego huu wa umaskini. Kemathi alipenda kula katika hoteli ya Sunrise. Mara tu alipofika kwenye hoteli hii, hakukuwa na haja ya kumuuliza chakula alichokitaka. Wahudumu wa hoteli hii walikwishajua chakula alichoweza kugharamia. Yaani *githeri* ambacho kilikuwa chakula cha bei ya chini zaidi katika hoteli hiyo.

Waaidha, Kemathi alipompeleka Kagendo hospitali kujifungua, jambo lililotawala mawazo yake lilihusu njaa kubwa ya pesa aliyokuwa nayo. Aliitajika kulipa ada ya shilingi elfu saba. Akiwa katika hoteli ya Sunrise, alijiuliza maswali mengi kuhusu mahali ambapo angezipata pesa hizo. Aliitulizia macho sahani nyeupe ya Sunrise huku akizikuna ndevu zake. Sahani hiyo tupu haikuwa na dalili zozote za kumpa suluhisho la matatizo yake.

Vile vile mtunzi anatusimulia kuwa kutokana na umaskini, watu wengi jijini Nairobi walikuwa hawawezi tena kugharamia chakula cha mchana . Hivyo, walizoea kwenda kujilaza kwenye nyasi katika bustani kama vile Jeevanjee na Uhuru ili kupitisha wakati

(uk. 73). Kulikuwa na uhaba wa kazi kiasi kwamba hata wale wenye digrii walikosa kupata kazi kwa urahisi. Hata wale wachache waliobahatika kupata kazi hawakulipwa vizuri na uwezekano wa kufutwa ulikuwa mwingi.

Muthomi, rafikiye Kemathi, anakiri kwamba umaskini umewafanya wanajamii wengi kuzama katika madeni. Hawawezi kugharamia maisha yao kuanzia mavazi hadi chakula, kwa sababu hayaoani na uhalisia wa mazingira yao. Anasema:

> Mimi ni Ofisa wa kiwango cha juu, lakini mshahara wangu ni shilingi elfu kumi! Nataka kula vizuri, kuvaa vizuri, kuishi nyumba nzuri, kununua televisheni, gari,--niambie jinsi nitakavyoyamudu yote hayo kwa shilingi elfu kumi? (uk.73).

Wamitila (2002:182) akizungumzia uhakiki wa Ki-marx, anasema kwamba, U-marx unahusu nyanja mbalimbali kama uchumi, historia na jamii. Historia ya maisha ya binadamu inaweza kuelezeka katika misingi yakinifu ya kiuchumi. Misingi hii inachunguza njia za uzalishaji mali pamoja na miundo ya kiuchumi inayoathiri sio uzalishaji mali hiyo tu bali na usambazaji wake. Suala hili la uzalishaji mali na usambazaji wa mali hiyo linaunda kile ambacho hujulikana kama 'msingi.' Kwenye msingi huu ndiko kunakotegemezwa muundo wa juu au 'kikorombwezo.' Kikorombwezo ndicho kinachohusisha maadili, itikadi, dini na utamaduni.

Maelezo ya hapo juu, yanatuelekeza kwa chanzo cha utabaka katika jamii. Sifa za watu wa tabaka la juu zinaathiriwa kwa kiasi kikubwa na tabaka la chini. Tabaka la chini linaathiri vipengele vyote vya maisha ya jamii. Binadamu hulazimika kujiunga pamoja ili kuzalisha mali katika harakati zao za kuyakidhi mahitaji ya kimsingi. Muungano huu huwa na ugawaji wa majukumu ambayo ndiyo msingi wa kuundwa kwa matabaka katika jamii. Hatua ya juu ya mwendeleo huu ni uzukaji wa mfumo wa ubepari. Katika mfumo huu, mali inamilikiwa na idadi ndogo ya watu. Watu hawa wanapata mali yao kutokana na unyonyaji wa umma na hasa wafanyikazi.

Nadharia ya Maadili inapinga mfumo huu wa ubepari kwa kushikilia kwamba kila mtu afanye kazi. Kufanya kazi huchukuliwa kama jukumu la kila mtu alilopewa na Mungu ili aweze kujikimu wala sio jukumu la wachache. Hivyo, wafanya kazi wote waungane katika kupinga utabaka, ukandamizaji na kunyimwa haki.

Marx aliainisha jamii ya kibepari katika matabaka mawili: mabwanyenye na wafanyikazi. Tabaka la mabwanyenye ni la matajiri. Wazalishi mali wenye mashamba, ardhi, viwanda na kadhalika. Nao ni kundi ndogo lakini wanamiliki kila kitu. Tabaka la wafanyikazi ni la maskini, ni la wafanyikazi mashambani, viwandani na ni walinzi wa mali za matajiri. Tabaka hili ndilo lenye watu wengi. Maskini wanatoa jasho kuzalisha mali lakini malipo yao ni duni. Hawalipwi wanavyostahili, wananyonywa, wanauza nguvu zao kazini lakini ujira ni duni. Ni mfumo unaokwenda kinyume na nadharia ya Maadili na unaowafanya maskini kuzama katika umaskini huku matajiri wakizidi kupata faida na utajiri zaidi.

Uovu kama vile ufisadi, ukoloni na dhuluma ya unyonyaji unachangia pakubwa katika kuleta athari ya utabaka. Jamii ya Upotevu ilikuwa imeathiriwa na utabaka. Mwandishi wa riwaya ya *Upotevu* anatuarifu kuwa mitaa duni kama Dandora na Tufani ndimo walimoishi wafanyikazi wengi jijini Nairobi. Wasiokuwa na kazi, waliofanya vibarua na wenye kazi za kijungu jiko kama za uyaya na ulinzi wa mali za watu. Waliishi katika hali mbaya zaidi. Hao, na ndio waliokuwa wengi, waliishi katika madongoporomoko kama vile Mathare, Kawangware na Kibera. (uk. 87)

### 4.2.0 Vifo

Kutokana na uovu unaowakabili wahusika katika jamii ya mwandishi wa riwaya ya *Upotevu,* tunashuhudia vifo ambavyo vingeweza kuepukika. Uhai ni kitu cha thamani na unafaa kulindwa kwa vyovyote vile. Baadhi ya maovu tunayoyaona miongoni mwa watu duniani yana hatima yake katika kifo.

Asili ya kifo cha Flora ni kupandwa na ghadhabu baada ya kumfumania mpenzi wake Chabare akizini na mhudumu wa nyumbani wa jirani yao. Hili ni jambo ambalo Chabare hakutaka kulisema wazi wazi kwa kuhofia athari zake. Kemathi alifichuliwa siri hii na Keremi, nduguye Chabare. Usiku huo wa siku ya Chabare kufumaniwa na Flora akizini, wawili hao waligombana karibu usiku kucha. Flora alizungumza kwa ukali na uchungu mwingi, na maneno yake yalikatizwa mara kwa mara na kilio cha kwikwi. Keremi anasimulia:

> Niliporudi nyumbani siku hiyo, nilikuta ugomvi
>
> baina ya Flora na mpenzi wake umechacha. –
>
> --Nilipoingia kitandani kulala, bado ugomvi

> ulikuwa unaendelea. - - - Sina shaka kuwa
> Flora alijiua keshoye kutokana na ugomvi huo.
> (uk.114).

Katika sura iliyotangulia hii, tumeeleza kwamba Chabare alipenda sana mambo ya wanawake. Flora naye, ingawa alikuwa rafikiye Chabare, alikuwa na wanaume wengine wengi. Ukware wa wawili hawa unasababisha kifo cha Flora na hivi karibuni, tutaona utakavyosababisha kifo cha Chabare mwenyewe. Kisa hiki kinatupelekea kutomlaumu Chabare peke yake kwa sababu Flora ni mwenye tabia yiyo hiyo anayoikashifu.

Kwa mujibu wa Thungu Jane et al (2008:162), malezi anayoyapata au anayoyakosa mtoto, yana athari chanya au hasi katika maisha yake ya utu uzima. Wanasaikolojia wanadai kwamba maadili ya mtu yanafaa kujengeka akiwa katika umri kati ya miaka (0--12). Kupitia kwa kinywa cha Kemathi, mtunzi wa kazi hii anatueleza kuwa Flora alikuwa na matatizo ya kisaikolojia yaliyotokana na malezi yake (uk. 114). Flora hakuwa mtoto wa Ngotho wa kuzaa, mamake akiolewa, tayari alikuwa naye. Flora hakupata malezi bora, maisha yake ya utotoni yalijaa madhila na misukosuko.

Isitoshe , mamake Flora alikufa akamwacha, hivyo, Flora aliyakosa malezi muhimu pamoja na upendo kutoka kwa wazazi wake. Pengo hilo ambalo halikuzibwa lilimwathiri vilivyo katika siku zake za baadaye. Yale mapenzi ambayo aliyakosa akiwa mtoto yalimpelekea kujiona kama kiumbe asiyefaa na ambaye hapendeki na yeyote duniani. Mapenzi hayo ndiyo anayoyatafuta kwa dhati.

Vile vile, babake Flora hakuwajibika katika kumlea Flora, pesa zake zote ziliishia ulevi, hakuwapenda wanawe na hata kushindwa kuwasomesha. Kemathi anamweleza Keremi kwamba:

> Mtu mwenye silika kama ile ya Flora angejiua tu kwa sababu moja au nyingine. Hata kama hakumfumania Chabare akizini na mtumishi wa nyumbani, angepata jambo jingine maishani la kumkasirisha na kumchochea kujiua. (uk.114).

Yote haya yanatuthibitishia kwamba Flora aliyapitia matatizo mengi katika ukuaji wake na athari hizi hasi zinazomwandama hazingeweza kuepukika.

Chabare naye aliuliwa akiwa kwenye mazishi ya aliyekuwa mpenzi wake, Flora, katika shamba la babake huko kwao Murang'a. Baada ya kifo cha Flora, kulizuka ugomvi mwingi pamoja na migogoro isiyokwisha kuhusu kwanza; chanzo cha kifo cha Flora. Pili, ulipaji wa bili ya hospitali iliyoachwa na Flora huko Ramesh. Chabare aliwataka wazazi wa Flora na jamaa zao kulipa kiasi cha pesa zilizobaki. Ngotho alikataa kata kata pendekezo hilo huku akitishia kuwa ikiwa Chabare angekataa kulipa pesa hizo, angekiona cha mtema kuni. Ugomvi huu uliwapelekea wahusika wa familia hizi mbili kutusiana na kutishiana vikali hadharani pasipo na kujua maafa ambayo yangetokea hatimaye.

Baadaye, Ngotho na mwanawe Ndung'u walikwenda kuripoti kwa Polisi kuwa walimshuku Chabare kwamba alihusika na kifo cha Flora. Kitendo hiki kilileta athari hasi kwa kusababisha chuki ambayo ilizaa uovu zaidi baadaye. Tunaambiwa:

> "Mtu ambaye atalipa pesa hizo si mwingine bali ni wewe Chabare, upende usipende!" Ndung,u alichangiza. "Basi tutaona kama ni Chabare atakayezilipa, au kama ni nyinyi," Keremi alisema kwa sauti iliyojaa mori. (uk. 105)

Baada ya familia hizi mbili kushindwa kuafikiana, Mburugo, nduguye Chabare ambaye ni mwanajeshi aliamua kuingilia kati na kuumaliza mzozo kuhusu kifo cha Flora. Mburugo alimwagiza mkuu wa hospitali aiachilie maiti ikazikwe na bili ya hospitali adaiwe babake Flora. Mkuu wa hospitali aliingiwa na hofu kwa vile Mburugo alikuwa amevalia sare ya jeshi, akakubali. Ngotho alipigiwa simu na kulazimishwa kuchukua maiti akaizike na baadaye alipe bili yote ya hospitali. Tunaelezwa kwamba: "Ngotho alikasirika sana kwa kulazimishwa kulipa bili yote ya hospitali peke yake, akaapa kwamba angewachukulia hatua kali mahasimu wake." (uk.147)

Chabare na nduguye Keremi walikwenda kuhudhuria mazishi ya Flora huko Murang'a. Baada ya mazishi, Ngotho alianza kuwahutubia watu, akiwaambia kuwa 'mwanawe aliuawa na mwanamume aliyekuwa akimchumbia, akishirikiana na jamaa zake.' Matamshi haya

yalileta athari mbovu hivi kwamba yaliwafanya waombolezaji kuwapiga Chabare na Keremi huku Chabare akiuwawa na Keremi kubakia katika hali ya mahututi.

Ufisadi ni uovu. Kifo cha babake Kemathi kilisababishwa na ajali ya barabarani. Kemathi anapotathmini kuhusu kifo cha babake, anaona kuwa kiini cha tanzia hii ya kifo kilichotokana na ajali barabarani ni biashara ya matatu. Anasema: "Pingu za ufisadi ziliwafunga mikono maafisa waliokuwa na wajibu wa kutekeleza sheria za barabarani." (uk.79).

Ni bayana kwamba maafisa wa polisi ambao wangetekeleza wajibu wao wa kuhakikisha kwamba magari yaliyo barabarani si mabovu na yanaendeshwa kwa utaratibu, wamefungwa na pingu za ufisadi. Ufisadi wa aina hii una athari hasi hivi kwamba unasababisha vifo vya wananchi wasio na hatia na kuacha jamaa zao zikiathirika vikali kama inavyodhihirika katika kazi hii.

Gari lililomuua Nabea lilikuwa linaendeshwa kwa mwendo wa kasi katika barabara ya lami. Pia Motethia na familia yake yote waliangamia katika ajali ya barabarani. Majeruhi wanaonusurika vifo vya ajali barabarani nao ni wengi, kwa mfano, mamake Oki-Ojok.

Kifo cha mzazi huwa ni pigo kubwa sana kwa jamaa nzima. Nabea alikuwa kiunganishi cha familia yake na hata kijiji, aliwafanya watu kuona thamani ya ujamaa. kifo chake kiliashiria kupita kwa enzi ya furaha na kubisha enzi iliyojaa migogoro. Kuna utengano katika familia yake, Kemathi alipokwenda nyumbani wakati wa Krismasi, anamkuta mamake akiwa amechutama peke yake jikoni. Anamuuliza; "Mbona uko peke yako, mama?" "Wengine wako wapi, mama?" Kisha mamake alimjibu; "mwanangu, baada ya babako kutuacha,

ushirikiano umefifia hata katika familia yetu yenyewe. Getonga na Moronge walijitenga nasi." (uk. 139). Hivyo, kifo cha babake Kemathi kilileta huzuni mwingi na hata kuacha makovu katika nyoyo za watu wa jamaa yake. Upeo wa athari hizi ni mpana kiasi kwamba Kemathi alipokwenda kulala, aliota kuwa Getonga na Moronge wanauvunja mlango kwa mawe. Kisha wakamwingilia chumbani na kumkatakata vipande kwa upanga.

### 4.3.0 Hofu ya Kimaisha

Hofu huletwa na vitisho, kubaguliwa, kunyimwa haki, upweke, utengano pamoja na vitendo vya kikatili kama vile mauaji, kupigwa, kukanwa, kutusiwa na kuteswa au kusumbuliwa. Ngotho na mwanawe Ndung'u walikwenda Polisi kuripoti kwamba Flora aliuawa. Asubuhi moja Chabare akiwa nyumbani kwake akiwa na Kemathi pamoja na Keremi, waliingiliwa na Polisi. Askari hao waliwababaisha vijana hao huku wakiwatisha na kuwataka Chabare na Keremi kufika kwenye kituo cha Polisi cha Kasoko wakati wa mchana siku hiyo. Polisi hao walitaka kwenda kuwadadisi vijana hao kuhusu chanzo cha kifo cha Flora. Mwandishi anatuelelza kwamba vijana hao waliduwazwa na kule kuingiliwa na askari Polisi kwa fujo asubuhi namna ile (uk. 99). Vijana hawa walishikwa na wasiwasi na woga kutokana na hofu kwamba kifo cha Flora kingezua balaa. Chabare anamwambia Kemathi kwamba: "Kama ulivyosema Kem, sasa kuna uwezekano wa kutokea mashaka makubwa zaidi kwa sababu ya mambo haya kupelekwa kwa Polisi." (uk. 100)

Hii ni ithibati kwamba vijana hawa wameathiriwa na wasiwasi mwingi ambao umewaacha katika hofu ya namna hii. yote haya ni matokeo ya moja kwa moja ya uozo. Keremi

aliwaona Ngotho na mwanawe Ndung'u kama mashetani ambao walifurahia kuwaingiza watu wengine mashakani.

Pamela Kagendo, rafikiye Kemathi, alishika mimba akiwa chuoni. Tatizo la wanafunzi kupata mimba wakiwa chuoni lilikuwa kubwa kuliko kosa lingine lolote na lingempelekea mwanafunzi kufukuzwa hata kama alibakisha siku moja tu kumaliza masomo yake. Jambo hili lilimwathiri Kemathi kiasi cha kuwa na wasiwasi muhula mzima huku akihofia mustakabali wa mchumba wake.

Waaidha, tangu kutokea kwa kifo cha Flora, tunamwona Chabare akiwa na wasiwasi kuhusu mkondo wa matukio sasa. Tanzia ya kifo cha Flora haikumwathiri Chabare tu bali na hata jamaa za Flora na Chabare pamoja na rafikize Flora kama Kagendo. Keremi alipigwa na Polisi na kutishwa kuwa yeye ni mshukiwa katika kesi ya mauaji ya Flora. Jambo lililowafanya Keremi na Kemathi kupata mshangao zaidi. Wakiwa kwenye mazishi, Keremi pia alipigwa na waombolezaji. Pamela Kagendo alipoarifiwa kuhusu kifo cha rafikiye Flora, mwili wake ulitikisika kwa mshtuko. Tanzia hiyo ilimwathiri vikali na kubakia katika hali ya kuachama. Kando na hayo, Kemathi alipopata habari ya kifo cha rafikiye Chabare kutoka kwa Mburugo, alisikitika sana, akawa anazungumza kwa shida. Mwandishi anasimulia kwamba, habari za tanzia alizopokea Kemathi zilikuwa pigo kubwa sana kwake. Alitiririkwa na machozi huku matone kadha mazito yakianguka kifuani mwake. (uk.149)

## 4.4.0 Athari za Ukoloni

Kabla ya majilio ya wakoloni barani Afrika, Waafrika walikuwa na elimu yao na tamaduni zao. Kuja kwa wakoloni katika Afrika kumeleta mabadiliko mengi miongoni mwa Waafrika. Mwafrika aliathirika sana na tamaduni za Mzungu na hivyo kuiga matendo na tabia za Kizungu. Flora na Chabare ni mfano wa Waafrika wenye tamaa ya vitu vya Kizungu huku wakidharau vyao.

Chabare na Flora wanayathamini maisha ya jiji kwa kuwa yana nafasi kubwa ya kujifurahisha kama vile uwepo wa viburudisho kuliko mashambani. Wanaona tamaduni za Kiafrika kama za kuwarudisha nyuma na kuwanyima starehe. Wanawaona wale wanaoshikilia tamaduni hizo kama washamba na wasiokubali mabadiliko. Flora ameathiriwa na mambo haya ya kigeni kiasi cha kusema kuwa nyumbani kwao kumejaa ushamba na ushenzi. Hali hii inakaribiana sana na ile tunayoipata katika tamthilia ya *Amezidi* ya Mohamed (1995). Mari, amesawiriwa kama mhusika aliyejaa kiburi na mwenye dharau kwa tamaduni za Waafrika. Ni mhusika ambaye kwake tamaduni za kiafrika ni ujinga na hauna ustaarabu.

Athari hizi za ukoloni zimewafanya Waafrika wengi kujiweka katika viwango vya ubora ambavyo vinaenda kwa misingi ya Kizungu. Kiingereza ni lugha ambayo Waafrika wengi wanaipenda na mara nyingi hutaka kunasibishwa nayo kuliko lugha zingine za Kiafrika. Baada ya kujinyakulia uhuru, waliithamini na kujionyesha kwayo kwa madaha. Mwandishi wa *Upotevu* amemsawiri Ngotho kama Mwafrika aliyeathiriwa na tabia hii. Wakiwa kwenye mkutano wa kupanga mazishi ya Flora, Ngotho anajikaza kutumia Kiingereza ambacho

kinamtatiza kwa kutokimudu vizuri huku akiiacha lugha ya Kiswahili ambayo aliifahamu kuliko Kiingereza na iliyoeleweka na wote waliokuwa katika mkutano.

Jamii inayosawiriwa na mtunzi wa riwaya ya *Upotevu* inapatikana katika nchi iliyokuwa ikitawaliwa na wakoloni lakini sasa imekuwa huru. Ajabu ni kwamba, hata baada ya uhuru mambo ni yale yale. Uhuru huo ni jina tu, hapana mabadiliko wala dalili za kuwepo kwa mabadiliko. Serikali za kikoloni zilitumia mabavu kutimiza haja za kibinafsi. Askari wa kikoloni waliwapiga Waafrika ili kuwatia woga na kuwafanya wasipiganie haki zao. Mfumo huu wa utawala potovu ulirithishwa kwa askari wa serikali za baada ya ukoloni na athari zake hasi kama vile raia kuwachukia polisi, kuwapiga raia ovyo ovyo n.k, zinadhihirika katika jamii zetu kila mara.

Chabare aliposhikwa na Polisi kwa kushukiwa kuwa alihusika na kifo cha Flora, Keremi alikwenda karibu naye huku akitaka kuuliza sababu ya kushikwa. Tunaambiwa kwamba:

> Askari aliyekuwa amemshika Chabare mkono
> wa kulia alimbaka Keremi kwenye kisogo,
> akamvurumisha kwa nguvu. Aliangukia
> makalioni kwa kishindo."Mjinga hii! ya nini
> unakuja kushikashika huyu? Hapana
> jua ni mahabusu?" askari alibweka. (uk. 117)

Hii ni ithibati kuwa askari hawa wameathiriwa na mfumo wa kimabavu usiowaheshimu wananchi. Mabadiliko yaliyotarajiwa baada ya uhuru hayaonekani. Askari hao pia wamesawiriwa kuwa wenye fujo na ujeuri. Mwandishi anasema kuwa walipokwenda kwa nyumba ya Chabare, walibisha mlango kwa ujeuri kisha wakaupiga mateke hadi ukafunguka kwa kishindo. Raia wengi waliwachukia Polisi kwa sababu ya dhuluma zao kwa wananchi. Kila mara, jina 'Polisi' lilipotajwa, kulizuka wasiwasi mwingi miongoni mwa wananchi. Hivyo, ni kweli kuwa hata baada ya uhuru Polisi hawakufunzwa maadili faafu.

### 4.5.0 Kutowajibika

Kutowajibika ni ile hali ya mtu kutotekeleza majukumu anayopaswa kuyatekeleza. Mwandishi anatuonyesha viwango tofauti tofauti vya kutowajibika katika jamii yake kwa kutumia wahusika. Maovu mengi yapatikanayo katika jamii k.v anasa, ulevi, tamaa na ufisadi huwapelekea watu fulani kuzembea katika kutekeleza majukumu yao kama vile kupeana malezi yanayostahili, kukosa kuwa vielelezo bora kwa wategemezi, kutotumia rasilmali ya umma ipasavyo.

Kutowajibika hakuwaathiri waliokosa kuwajibika tu, bali huwaathiri na watu wa familia zao na hata wanaowazunguka. Kutowajibika huleta hasara nyingi kama kurudisha maendeleo ya binafsi na nchi nyuma, watoto kukosa masomo, familia kutaaabika, kupata magonjwa na kadhalika. Ni mambo ambayo yanaweza kuzuiliwa iwapo watu watakuwa waangalifu na waaminifu.

Tunamwona Flora akiwa na matatizo mengi katika utu uzima kwa sababu wazazi wake walikosa kuwajibikia malezi yake akiwa mtoto. Ngotho alikosa kumlipia mwanawe Flora karo ya shule. Mzazi huyu hakukosa pesa, mapato yake yote aliyatumia kwa ulevi. Ndung'u pia, alisoma hadi darasa la saba tu, na kukosa kuendelea na masomo yake kwa sababu ya kutolipiwa karo na babake Ngotho. Kutosoma huku kunamfanya ashiriki katika maovu mengi kama yanavyojidhihirisha riwayani: ulevi, kutumia lugha chafu, ugomvi, kupigana, na hata tunaambiwa kuwa yeye ndiye aliyemuua Chabare.

Nadharia ya Maadili inalenga kuchanganua kilichomo ndani ya vitendo ambacho huvifanya vitendo hivyo kuwa sawa au kutokuwa sawa. Wahusika wengi ambao tumewachunguza katika kazi hii, wana vitendo viovu. Matendo hayo yanawaletea athari hasi katika maisha yao. Jambo ambalo linatufanya kuamini kuwa vitendo viovu vinawaelekeza watu kwenye upotevu.

Mtunzi anaonyesha kuwa wazee wengi wamepotelea kwa 'ndogondogo' na kukosa kutimiza mahitaji ya kimsingi kwa familia zao. Kuna familia nyingi ambazo zimeathirika vibaya kwa sababu ya wazee kutumilia mapato yao yote kwenye ulevi. Akina mama na watoto hawapati haki yao. Katika kilabu ya Ndototamu kuliko tafrija, wasichana warembo walijiegemeza kwenye kuta, wakijaribu kuwavutia wanaume ambao walikuwa wanaingia. Wazee walipoingia ndani na ndogondogo hao kujitumbuisha, ngoma ya Rashid Kombo ilipaa angani kama ilivyo hapa chini.

Enyi wazee wa kisasa

Wenye mali na mapesa

Mwatamani ndogondogo

Ndogondogo si kidogo

Watakacho si kidogo

Pesa zateketea

Familia zapotea

Wazee ----------- ee

Vijana ----------- aa

Mtakuja kupotea (Uk. 60)

Hapa, mwandishi anadhamiria kuonyesha kuwa ndoa zimeathiriwa na uozo usio haba katika takriban nyanja zote. Hata asasi kama ndoa ambayo inatarajiwa kukuza maadili na kuwa kielelezo bora cha watoto wanaokua imezama katika uovu. Wasichana ambao wanatajwa kama 'ndogondogo' huenda ikawa wamekosa kutulia nyumbani kwa sababu wanaiga tabia za wazazi wao, kwani hawakupata malezi wala vielelezo bora. Wazee hao pia wamekosa kuwajibika kwa sababu wanakesha vilabuni na kukosa kutimiza wajibu wao wa ndoa nyumbani. Ni bayana kuwa wimbo unasawiri picha halisi kuwa; pesa zateketea, familia zapotea. Atakayezikomboa familia hizi ndiye hatumujui.

Ithibati nyingine ya athari ya kutowajibika imo katika kisa cha mzee jirani ya Kemathi, huko Dandora anakoishi. Mke wa mzee huyo alitoka nje akiwa nusu uchi huku akiwa amejifunga

leso ndogo kiunoni. Sehemu yote ya juu ya mwili wake ilikuwa wazi. Tunasimuliwa kuwa alipoketi, aliweka mguu mmoja huku na mwingine huko. Mbaabu alipomwona, alitamaushwa na tukio hilo. Alipomuuliza Kemathi sababu yake kufanya hivyo, alimjibu: "------- labda ana kusudi la kuwatega wanaume." (Uk. 21)

Inasemekana kwamba mwanamke huyu anatabia za kimalaya kwa sababu mwanaume aliyemwoa ni mume hivi hivi, bwege, anakesha katika vilabu vya pombe na ulevi wa kupindukia ulikwisha kumlemaza. Ni wazi kwamba mwanamume huyo hatekelezi wajibu wake wa ndoa, anazembea. Inaelekea kuwa mwandishi amekatishwa tamaa na ukweli kuwa mwanamke kama huyo ambaye ana watoto watatu hawezi kuwa kielelezo bora cha kuigwa na binti zake, ni mpotovu wa maadili. Isitoshe, Chabare anatoa maelezo kwa Kemathi kuwa Flora hakupata malezi bora. Anasema:

> Ngotho alikuwa mzee mchoyo na asiyewajali watoto wake. Mapato yake yote yaliyotokana na shamba lake kubwa la majani chai yaliishia kwenye pombe. Flora hakuwa mtoto wa Ngotho wa kuzaa. Mamake alipoolewa na Ngotho, tayari alikuwa naye. (Uk.109).

Dondoo hili linatuonyesha kwamba Ngotho alikosa uwajibikaji. Hakutoa malezi bora kwa wanawe. Sio kwa sababu Flora hakuwa mtoto wake wa kuzaa, mwandishi anasema kuwa hata wanawe wa kuzaa yaani Ndung'u hakupata utunzaji wowote. Alisoma hadi darasa la saba tu, na babake akakataa kulipa karo ndipo aweze kuendelea na masomo.

Vile vile, Vitendo viovu vya Chabare vinamfanya kudanganya kazini kuwa anakwenda kliniki ilhali anakwenda kujiburudisha na mpenzi wake Flora katika hoteli moja maarufu iliyoitwa Kwanjua. Mwandishi anasema:

> Chabare alifunga ofisi na kushika njia ya kuelekea River Road. Ujumbe aliomwachia sekretari ulikuwa wa kujisalimisha tu endapo wakubwa wake wangemhitaji. Hakuwa anaenda kliniki. Alikwenda kumpokea mpenzi wake, Flora Nyambura, aliyesafiri kutoka Murang'a kuja kumtembelea. (uk. 48)

Kutoroka kazini kwa sababu kama hizi zinazojitokeza kwenye dondoo hili hapa juu huathiri pakubwa uchumi wa nchi. Kuzembea kazini ni sababu mojawapo ya kutoendelea kwa mataifa ya Kiafrika. Hivyo, tunaafikiana na nadharia ya Maadili kwamba nchi za kupata maendeleo ni zenye raia waadilifu na wafanyikazi waliokuzwa katika misingi ya kiadili.

Mwandishi kupitia kwa mhusika Nabea, anatufunza kwamba mtu mzima anapaswa kufaidika kutokana na mawazo ya wenzake lakini sio kutawaliwa nayo. Mzee Nabea alikuwa mtu asiyeweza kutawaliwa na mawazo ya wenzake. Nabea alikuwa amezingirwa na marafiki wengi walioendeleza uozo. Marafiki zake wengi walikuwa na mitazamo na mielekeo tofauti kabisa na yeye. Ajabu ni kwamba Mzee Nabea aliweza kusimama imara kwa kujitegemea kimawazo. Hivyo, mhusika huyu ni kielelezo chema cha maadili anayefaa kuigwa kama inavyosema nadharia ya Maadili.

Tabia za kemathi na za wazazi wake zinalingana. Jambo hili linatupelekea kuamini kuwa aliathiriwa na yale matendo ya wazazi wake. Kemathi ni mwenye utu na maadili. Alipata malezi mema na hivyo kujifunza mambo mengi mazuri kutokana na wazazi wake. Kutia bidii kazini ilikuwa maadili aliyojifunza kutoka kwa wazazi wake. Alikuwa na bidii masomoni. Ana msimamo thabiti kama wa baba yake. Kwa mfamo, ana marafiki wengi wanaokunywa pombe lakini yeye hanywi.

Kwa upande mwingine, Kemathi alimwathiri Mbaabu. Aliweza kuwa kielelezo bora kwake haswa katika masomo. Alimshauri kuhusu tabia nzuri na kumtaka kutia bidii katika masomo. Kimani na Chimerah (1999:130) wakizungumzia maadili wanasema kwamba watu wote wanastahili kuwa na tabia nzuri, kwa hivyo, ni wajibu wa kila mtu mwenye tabia nzuri kuwalazimisha hao wenye matendo maovu kuyaacha, badala yake, kuwa watu wema, wenye tabia nzuri. Mbaabu alipomwandikia Kemathi barua anamweleza kuwa: "Mimi kwa upande wangu nimefuata ushauri wako, nimewapuuza ndugu zetu wakubwa na kuzingatia tu masomo yangu." (uk.131). Ili ni thibitisho kuwa Mbaabu alifuata nyayo za Kemathi. Aidha, Kemathi, katika uadilifu wake aliathiri maisha ya Maria kwa kumshauri na kuleta furaha pamoja na matumaini katika maisha yake ya upweke na yaliyojaa hofu.

Oki- Ojok ni mhadhiri wa Chuo Kikuu Cha Nairobi aliyewajibika kinyume na wahadhiri wenzake. Kemathi anasikitika kuwa hakuwahi kufunzwa na yeye chuoni. Waliobahatika kufunzwa naye walimsifu kuwa ni mhadhiri hodari, jasiri, mzalendo, mwadilifu na aliyewajibika kuliko wahadhiri wengine. Alikuwa mwandishi na mwaguzi wa jamii yake. Kwa kuathiriwa na maisha ya Oki-Ojok Kemathi ana azma ya kutetea haki ya wanyonge katika jamii. Jambo ambalo ananuia kulifanya kupitia kwa uandishi wa vitabu. Mwandishi

amemsawiri mhusika huyu hivyo ili aweze kuwa kielelezo bora cha uwajibikaji kwa wasomaji. Anazidi kusema kwamba Oki – Ojok ana itikadi na msimamo thabiti, alikataa kununuliwa na wanasiasa ndiposa walitaka kumwangamiza.

Nadharia ya Maadili inadai kuwa wasomaji wa kazi za fasihi wanapaswa kuiga tabia za wahusika wema na kuepuka tabia za wahusika waovu. Oki-Ojok ni mhusika anayefaa kuigwa.

Kupitia kwa mhusika Nabea, mwandishi anadhamiria kuielimisha jamii kuwa mafanikio hayaji hivi hivi bila watu kuwajibikia majukumu yao. Anasema kuwa mafanikio ya Nabea hayakujileta yenyewe. Yalitokana na bidii pamoja na kujitolea. Riwayani, ni dhahiri kuwa mzee Nabea alijinyima vitu vingi ili aweze kuwasomesha watoto wake. Katika juhudi zake zote hizi, wazee wa rika lake walizoea kumcheka kwa kutembea na nguo zenye viraka. Kauli hiyo inadhihirisha kuwa wazee hawa hawakuwajibikia majukumu yao. Mwandishi anasisitiza kwamba mapato ya wazee hao yaliishia kwenye pombe na anasa nyingine.

Kinyume na Mzee Nabea, watoto wake wa kwanza yaani Gitonga na Moronge walikosa kuwajibika. Tunaambiwa kuwa:

> Kemathi aliyaona matatizo mengi katika familia
> yao kama matokeo ya kaka zake kushindwa
> kusikilizana na kuwasaidia wazazi na ndugu zao.
> Daima walikuwa katika mashindano ya kutafuta
> utajiri . Hata karo ya Mbaabu walikataa kusaidia
> Kulipia.(uk. 38)

Jambo hili lilimlazimisha Kemathi kutoa sehemu ya marupurupu yake kusaidia katika kulipia kaka yake mdogo Mbaabu karo. Nadharia ya Maadili inayoongoza kazi hii inadai kuwa binadamu ana uwezo wa kujifunza utu na anastahili kuyajali na maslahi ya binadamu mwenzake, watoto wawili wa kwanza wa Nabea walikosa uwajibikaji na hivyo kutojali maslahi ya wadogo wao. Wanatenda kinyume na nadharia ya Maadili. Kwa hivyo, walikosa maadili na kudidimia kwenye uozo.

### 4.6.0 Magonjwa

Kusambaratika kwa huduma zilizotolewa na mamlaka za jiji kwa wakazi wake kulileta athari mbovu kwa wakazi wake. Dandora ulikuwa mtaa wa vibanda. Mabaki ya bidhaa zilizouzwa vibandani yalirundikana kila mahali yakazua vilima vya takataka. Uovu wa ufisadi ulikwisha kuwafunga macho wale ambao wangefuatilia utekelezwaji wa huduma hizi za kuondoa takataka. Ndiposa maradhi ya kipindupindu na homa ya matumbo yaliwapata wakazi wa jiji mara kwa mara.

Kagweria anatusimulia kwamba vijana waliojihusisha na uovu wa ukahaba, walikuwa katika hatari ya kupata ukimwi. Ugonjwa ambao haukuwa na tiba. Hii ndiyo baadhi ya mitego aliyojaribu kujiepusha nayo Kagweria, kwa kuwa mwadilifu ili kujiepusha na athari za magonjwa ya zinaa na athari hasi za maovu mengine. Pamela Kagendo anatueleza pia kwamba, akiwa shuleni, wasichana wengi wa rika lake walipata na kuavya mimba, jambo ambalo analieleza kuwa ni hatari katika enzi hii ya ukimwi.

## 4.7.0 Vita

Mara nyingi ugomvi unapokithiri, husababisha vita ambavyo huwaacha watu katika matatizo mengi. Chabare, Flora, Maria, Muthomi na Kemathi wakiwa katika burudani zao huko Ndototamu, kulizuka vita kati ya Maria, na Flora na Chabare. Chabare alipocheza densi na Maria, Flora alikasirika na kuanza uzushi. Ugomvi huo uliposhika kasi, Maria alimrukia Flora, akamzaba vibao mashavuni, akampiga teke tumboni na kumwangusha chini. Kisha akamwinamia na kumpiga makonde kadha wa kadha. (uk. 62)

Chabare alipoona mpenzi wake akiadhibiwa, alimchupia Maria, akampiga ngumi ambayo illmfanya Maria kumrushia Chabare mateke ya karate na kumwangusha chini. Mtunzi anasimulia kwamba: "Maria alipigana kama mtu aliyefunzwa na kuhitimu kazi hiyo." Vita hivi viliwapelekea Chabare na Flora kushikwa na Polisi na kutiwa rumande. Athari hii ina chanzo chake katika Flora kumtusi Maria, kwa kumwita Malaya.

Flora alipokufa, starehe kati ya Chabare na Flora ziligeuka kuwa majonzi. Tunamwona Chabare akiitwa katika kituo cha Polisi kwa kutuhumiwa kuhusika na kifo hicho. Kufika huko, alidadisiwa kidogo, akatiwa pingu, kisha akaingizwa rumande. Kando na hayo, ufidhuli wa Polisi unawafanya kumpiga Keremi anapojaribu kuwauliza yaliyotukia. Baada ya Keremi kupigwa na kutupwa chini na askari, Kemathi na Keremi waliathiriwa sana na mabadiliko ya ghafula yaliyokwisha tokea. Waliamua kurudi nyumbani huku wakiwa katika hali ya bumbuazi.

## 4.8.0 Kukata Tamaa

Athari nyingine ya uozo katika jamii ni kukata tamaa. Huletwa na hali ambapo mtu hukabiliwa na matatizo na kukosa kuyatatua. Keremi amekata tamaa kutosikitikia ukware wa Chabare. Kemathi alipotaka kujua kilichompelekea Flora kujiua, Keremi alimsimulia hadithi ndefu kuhusu tanzia hiyo ya kifo. Tunaambiwa:

> Kemathi alitikisa kichwa kama ishara ya kusikitishwa na tabia ya Flora lakini hakusema lolote. Aliendelea kumsikiliza Keremi, uso wake ukionyesha hamu kubwa aliyokuwa nayo kuzisikia habari zaidi kulihusu hili fumbo la mwanamke lililoitwa Flora Nyambura. Kwa upande wake, Keremi alizungumza kama mtu aliyekwisha kata shauri kutosikitikia uozo wa kitabia wa Flora na Chabare. (uk. 112)

Dondoo linatuthibitishia kwamba Keremi alikuwa ameshuhudia uozo mwingi katika uhusiano wa Chabare na Flora na kuathirika kiasi cha kutojishughulisha tena na vitendo hivyo vyao viovu popote alipovishuhudia.

Isitoshe, Keremi alikuwa ameyavumilia mateso mengi kwa muda wa miaka miwili ambao walikuwa wamekaa pamoja na Chabare katika nyumba moja. Kwamba marehemu Flora, Christine na wapenzi wengine wa kakake, na pia Chabare mwenyewe, walipenda kuzikwepa

na kumwachia kazi zote za nyumbani, Kama vile kufua, kusafisha nyumba na kupika. Keremi alikuwa amechoshwa na uovu wa kakake na kuamua kuwa angehamia kwa nyumba yake. Kemathi alipojaribu kumkataza na kumshauri kuwa huenda Chabare akabadilika hivi karibuni, anakataa na kusema:

> "Haki ya Mungu mwakani sitaishi naye!" Keremi aliapa. "Nitatafuta hata kama ni chumba kimoja, nikodishe, nikae peke yangu." "Lakini labda atabadilika baada ya msiba huu, " Kemathi alipendekeza . Keremi aliangua kicheko cha kubeza. "Chabare abadilike? Labda Chabare mwingine, sio huyu ambaye ni kakangu. Flora alipokufa, Christine alikuja kuchukua nafasi yake usiku huo huo. Mapenzi baina ya Christine na Chabare ni ya kiendawazimu kama ilivyokuwa Flora alipokuwa hai. Sasa dalili za mabadiliko unayoyazungumzia ziko wapi?" (uk. 116)
> (Msisitizo wa mtafiti)

Kwa hivyo, tunaona kwamba Keremi alikuwa amekwisha poteza tumaini kuwa ndugu yake angebadilika. Haya yalitokana na uozo wake uliopita mipaka. Lililobaki sasa ni kumwacha aadhibiwe na ulimwengu.

## 4.9.0 HITIMISHO

Katika sura hii, athari za uozo kwa jamii zimebainishwa. Wanaoathirika zaidi kutokana na uovu ni wale wanaotekeleza uovu huo pamoja na wale walio katika mahusiano nao. Utafiti wetu umeonyesha kwamba maisha ya mwanadamu yanaharibika pale ambapo uozo unakithiri na kumdhuru kwa njia tofauti tofauti ambazo tumezichunguza. Vile vile, uozo una uwezo wa kumwangamiza binadamu kama inavyojitokeza katika tasnifu hii.

Asilimia kubwa ya wahusika katika riwaya ya *Upotevu* wameathiriwa kwa njia mbalimbali kutokana na uozo au kutokana na vitendo vyao viovu. Athari hasi zilizojitokeza ni nyingi mno kuliko athari chanya. Tumeuona uozo wa Chabare na Flora kwa mfano ukisababisha vifo vyao. Ni athari ambayo kwa kweli wangeiepuka iwapo wangekuwa waadilifu. Si hao tu, wahusika kama vile Ngotho, Ndung'u na Muthomi ni wapenda raha, wanashiriki katika ulevi wa kupindukia. Yote haya yanaleta athari mbovu kama ilivyoonyesha kazi hii.

Kutoteua lugha faafu kwa Ngotho kuliwachochea waombolezaji mpaka wakapandwa na ghadhabu kiasi cha kuanza kumpiga Chabare hadi kufa. Uovu ulionyemelea sekta ya biashara ya matatu unawaathiri wananchi wasiokuwa na hatia vikali. Maafisa walio na wajibu wa kutekeleza sheria za barabarani ni wafisadi. Matokeo yake ni ajali barabarani zinazowaangamiza raia wengi. Hivyo, utafiti huu umetuthibitishia kuwa uovu una uwezo wa kuyavuruga maisha ya mwanadamu na kumletea athari mbovu.

Imedhihirika vile vile kwamba, kukosa uwezo wa kuukabili uhalisi wa mambo huleta athari mbovu katika maisha ya jamii. Mambo kama umaskini, kutowajibika, magonjwa na vita yanaweza kukomeshwa iwapo mwanadamu ataukubali na kuufuata mfumo wa kimaadili na kujiepusha na uovu. Kimsingi, kinachohitajika ni ujasiri wa kuyakabili matatizo yanayowakumba binadamu na kuyatatua katika harakati za kujikomboa wao wenyewe.

# SURA YA TANO

## HITIMISHO

### 5.0.0 UTANGULIZI

Katika sura hii, tutatoa hitimisho la utafiti wetu. Sura yenyewe ina sehemu tatu muhimu. Sehemu ya kwanza inahusu muhtasari wa utafiti. Ya pili itashughulikia ufaafu wa nadharia tuliyoitumia. Sehemu ya tatu ina mapendekezo yanayokusudiwa utafiti wa baadaye katika kazi za kifasihi.

### 5.1.0 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Utafiti wetu ulikuwa na shabaha tatu. Shabaha ya kwanza ilihusu kuchanganua dhamira ya uozo katika riwaya ya *Upotevu.* Katika utafiti wetu tumegundua kuwa uovu ni wa aina nyingi. Tumeweza kuuainisha uovu katika makundi machache kama ilivyodhihirika katika kazi hii.

Uovu uliojitokeza zaidi katika kazi hii tuliyoihakiki ni uovu wa kimatendo. Uovu huu unajitokeza katika hali mbalimbali. Imedhihirika kwamba uovu huanza kwa hatua na kukua na kuzidi kukua hadi kiwango cha ukiukaji mipaka. Uozo unapofika kiwango hiki, matokeo yake huwa ni kuwepo kwa kizazi chenye kutawaliwa na uovu na ambacho kimedidimia katika upotevu. Taswira hii ya upotevu inajitokeza hata kwenye jalada na anwani ya riwaya yenyewe. Swala la uozo katika jamii limechukua nafasi kubwa katika jamii ya mwandishi.

Waaidha, utafiti huu umeonyesha kwamba chanzo cha uozo katika jamii ni ukosefu wa utaratibu maalum wa kimaadili. Nao upotofu wa maadili unaletwa na sera potovu, umaskini, uongozi mbaya, ukosefu wa vielelezo bora, kuasi utamaduni wa kiafrika na kupendelea mitindo mibovu ya nchi za kigeni n.k.

Kwa kuwa jukumu mojawapo la fasihi ni kusaidia katika kuielekeza jamii kutoka katika uoza hadi maisha mazuri zaidi, mwandishi wa kazi hii anajitokeza kuonyesha jamii iliyoyapatia maovu nafasi ya kusambaa na kuozesha jamii.

Lengo letu la pili katika utafiti huu, lilikuwa kuchunguza uhusika ulivyotumiwa kuendeleza uovu. Kazi hii imebainisha kuwa riwaya ya *Upotevu* ina wahusika wengi wanaochangia katika kuendeleza dhamira ya uozo. Tumebaini pia kuwa viwango vya uozo katika wahusika waovu vinatofautiana. Wahusika wanaoongoza katika kueneza uozo ni Chabare na Flora. Matendo ya wahusika hawa ni maovu kuanzia mwanzo hadi mwisho kama ilivyodhihirika. Wanapenda "kujistarehesha" kwa kushiriki katika uovu kama uzinzi, ulevi wa kupindukia, kuavya mimba na anasa za kila namna. Ni tabia ambazo kwao wanaziita usasa. Jambo lililotupelekea kung'amua kwamba hawatambui kuwa wamo katika upotevu.

Kwa upande mwingine, kupitia kwa wahusika kama Muthomi, Chabare, Kegonda na wengine, mwandishi anatusawiria wahusika waliosoma na hata kupata elimu ya chuo kikuu lakini ajabu ni kwamba, hawawi tofauti na wale ambao hawajasoma. Wamekosa utu, wana kiburi, ni wenye tamaa, matusi, wadanganyifu n.k. Elimu waliyoipata haionekani kuwasaidia wala kusaidia katika ukombozi wa jamii.

Kuna wahusika wachache ambao wanadhihirisha matendo ya uadilifu kama Nabea, Kemathi, Pamela Kagendo na Kagweria. Licha ya kuwa katika mazingira yaliyojaa uozo, wahusika hawa wanasimama imara dhidi ya shinikizo linalowavuta kwenye uovu. Kumaanisha kwamba wema unaweza kushinda uovu. Uvumbuzi huu umetufanya kuamini kuwa binadamu ana uwezo wa kujifunza tabia mbaya au nzuri apendavyo, ni jambo la uamuzi au hiari si majaaliwa.

Vile vile, tumegundua kuwa baadhi ya wahusika waliokosa vielelezo bora kwa mfano Ndung'u na Flora waliishia kuwa wahusika waovu. Kwa kutumia wahusika waovu na wema, mwandishi alitaka kutuonyesha vita vilivyoko kati ya uovu na uadilifu. Katika mgogoro huo, kazi hii imedhihirisha kuwa vitendo viovu vimechukua nafasi kubwa. Ni bayana pia kuwa baadhi ya uozo una chanzo chake katika uigaji wa mitindo mibovu ya kigeni. Inaelekea mwandishi alidhamiria kuwasuta Waafrika wanaoiga utamaduni wa kigeni bila kuuchambua. Okot P' Bitek akinukuliwa na Wafula na Kimani (2007: 118) anawakashifu Waafrika walioelimika akisema wao ni waigaji kwa kiasi cha kupotosha yale yanayoigwa.

Kutokana na matokeo haya, ni bayana kuwa madhumuni ya utafiti huu ya kuchunguza uhusika katika kuendeleza uovu yalitimizwa

Shabaha yetu ya tatu ilikuwa kubainisha athari za uovu katika jamii. Utafiti huu umebaini kuwa wahusika wengi waliodhihirishwa kama watenda maovu huandamwa na athari zisizoweza kukwepeka. Uozo wa Chabare na Flora ulioanza kwa hatua unaonekana kukomaa baadaye na kusababisha vifo vyao. Flora anajiua kwa kukosa kuvumilia uozo

aliouona, naye Chabare anapigwa kwa mawe na kufariki kwa sababu ya kutenda uovu. Mhusika Keremi amekata tamaa kuwa ndugu yake Chabare haonyeshi dalili zozote za kubadilisha tabia yake.

Imejitokeza kwamba maovu kama ulevi wa kupindukia, kushinda kwenye vilabu vya burudani na kutojali huwapelekea watu wengi kutowajibikia majukumu yao ya kimsingi. Familia zinahangaika kwa kukosa malezi na watoto wasipate vielelezo bora na hata kukosa elimu. Isitoshe, athari kama vile magonjwa mashaka na umaskini ni miongoni mwa matokeo ya uozo yaliobainishwa na utafiti huu.

Mwisho, utafiti huu umedhihirisha kwamba wahusika wengi waliosawiriwa wamekosa uwezo wa kuukabili uhalisi wa mambo kwa kutoshiriki katika utatuzi wa matatizo yanayowakabili. Tumeona pia kwamba uozo una uwezo wa kumwangamiza binadamu. Waaidha, suala nzima la mvutano uliopo kati ya wema na uovu huzalisha mgogoro kati ya nguvu zenye kuleta mafanikio na nguvu zenye kuzusha maangamizi. Hivyo basi, utafiti huu umetuthibitishia ukweli usiopingika kwamba uovu unaleta athari hasi katika maisha ya binadamu.

## 5.2.0 Ufaafu wa kinadharia

Nadharia tuliyoitumia ya Maadili inafaa katika uchanganuzi wa riwaya ya *Upotevu.* Mwandishi wa riwaya ya *Upotevu* anajitokeza kuwa mtunzi aliyekerwa na uozo uliopevuka katika jamii. Anaamua kuyaonyesha maovu hayo kupitia kwa utanzu huu wa kifasihi. Jukumu mojawapo la fasihi ni kuelimisha na kuonya wanajamii dhidi ya vitendo viovu. Mwandishi huyu anavuka mipaka ya kuangalia upande mmoja tu, ambao ni wema. Kama

mwandishi wa kifasihi, anawasilisha ukweli na uhalisi wa yale anayokumbana nayo. Madhumuni aliyonayo katika kuyafanya haya ni kutuonyesha kwamba ukiukaji wa maadili unadhuru.

Nadharia ya Maadili imetufaa kwa sababu ni nadharia inayoingilia na kuyachunguza matendo ya mwanadamu. Kazi tuliyoishughulikia ina vitendo vingi viovu kuliko vitendo vya uadilifu. Nadharia hii inashikilia kwamba tabia imejengeka vipande vipande, mwenye kuvipanga vipande hivyo sawa sawa vikaingiana na kuwa kitu kamili ndiye mwenye kupata maendeleo. Tumewaona wahusika wachache kama vile Kemathi waliojitahidi kukwepa vitendo viovu na kushikilia uadilifu. Wahusika hawa waliweza kuepuka madhara ya uozo. Kwa upande mwingine, wale waliojitoma katika uovu waliathirika huku maisha yao yakiyumbishwa hapa na pale na nguvu za maangamizi zipatikanao katika uozo. Hivyo, nadharia ya Maadili imetuwezesha kuyachambua matendo hayo na kuyaweka bayana.

Mwandishi anashiriki katika utatuzi wa matatizo yanayoikabili jamii yake kupitia kwa mapendekezo yake ya utawala mwema, upanuzi wa kiuchumi, na ugawaji wa rasilmali kwa njia ya haki, kuwepo kwa vielelezo bora katika malezi na uzingatifu wa maadili kwa jumla.

## 5.3.0 Tafiti za Baadaye

Katika utafiti wetu, tumejibana zaidi katika upande wa maudhui yanayoendeleza uozo. Tumegusia fani tu pale ambapo ilitusaidia kutilia mkazo dhamira ya uozo. Ni mapendekezo ya mtafiti wa kazi hii kwamba utafiti wa baadaye uchunguze suala la fani katika riwaya ya *Upotevu* kwa sababu pana mwingiliano mkubwa kati ya fani na maswala yanayoibuliwa na riwaya hii.

Utafiti huu ulijifunga katika kulichunguza suala la dhamira ya uozo katika riwaya ya *Upotevu.* Tunapendekeza utafiti mwingine uchunguze suala hili katika riwaya zingine za mwandishi huyu ili kuweza kubainisha jinsi ambavyo uovu umejitokeza katika kazi hizo.

# MAREJELEO


Barber, C.R (1976) *Good News Bible.* Glasgow: Collins Sons & Co. Ltd.

Kenyatta, J. (1978) *Facing Mount Kenya: The Tribal Life of The Gikuyu.* Nairobi:Heinemann Publishers.

Mogare, F. (2002) Uhakiki wa Tamthilia ya *Amezidi* kama kazi ya Kibwege. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi: Haijachapishwa.

Mong'eri, B.W.(2000) Utetezi Wa Maadili katika Fasihi-Nathari ya Shaaban Robert. Tasnifu ya M.A. Chuo kikuu Cha Nairobi: Haijachapishwa.

Mohamed, S.A. (1995) *Amezidi.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Muindi, A. (1990) Usawiri wa Wahusika Makahaba Katika Vitabu vya Said Mohamed. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Kenyatta: Haijachapishwa.

Mbatiah, M. (2000) (Mh) *Mwenda Wazimu na Hadithi Nyingine.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

__________ (2001) *Kamusi ya Fasihi.* Nairobi: Standard Textbooks & Graphics Publishers.

__________ (2004) *Wimbo Mpya.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

__________ (2005) *Upotevu,* Nairobi: Phoenix Publishers.

__________ (2006) *Migogoro.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

__________ (2007) *Vipanya vya Maabara.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

__________ (2007) *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine.* Nairobi: Focus Publications.

__________ (2010) *Msururu wa Usaliti.* Nairobi: East African Educational Publishers.

__________ (2012) *Majira ya Tufani.* Nairobi: Longman Publishers.

Mdee J. *et al.*(2011) *Kamusi ya Karne ya 21.*Nairobi: Longhorn Publishers.

Mlacha, S.A. na Madumulla J. (1996) *Riwaya ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Kimani N. na Chimerah, R. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.*Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nkonge, G. (2006) Athari za udhanaishi katika *Kichwamaji* na *Nguvu ya Sala* Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Okombo, P.L. (2011) Sitiari,Taashira na Tashibiha Katika Uwasilishaji wa Dhamira Katika *Utenzi wa Tambuka.*Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Nairobi: Haijachapishwa.

Robert, S. (1968) *Adili na Nduguze.*London: Thomas Nelson and Sons Limited.

_________(1968) *Utubora Mkulima.*London: Thomas Nelson and Sons Limited.

_________ (1968) *Siku ya Watenzi Wote.*London: Thomas Nelson and Sons Limited.

Thungu, J. *et al.* (2008) *Mastering PTE Education.* Nairobi: Oxford Publishers.

Timmons, M. (2002) *Moral Theory: An Introduction:* U.S.A: Rowman & Littlefield Publishers.

TUKI (2006) *English swahili Dictionary,3rd Edition.* Dar es Salaam: Institute of Swahili Research.

Wafula,R.M. na Kimani,N.(2007) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K. (2002) *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele vyake*, Nairobi: Phoenix Publishers.

________ (2003) *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Publications.

________ (2008) *Kanzi Ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.*Nairobi: Vide – Muwa Publishers.